Jarida la
MIFUGOUVUVI
Toleo la Septemba, 2020

# RAIS MAGUFULI AIPONGEZA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI











# Yaliyomo


- Rais Magufuli aipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi............ 1



- Baraza kuwaondoa Madaktari feki kwenye Sekta ya Mifugo............ 3
- SADC kutathmini athari za COVID 19 katika Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi............ 5
- Wizara yajipanga kutokomeza magonjwa yanayoathiri Mifugo ............ 7
- Wazalishaji wa Maziwa wahimizwa kutumia Masoko Rasmi............ 9
- Kampeni ondoa Magogo kwenye Mabucha ni endelevu: Msajili wa Bodi............ 12
- Wafugaji na Wavuvi wawezeshwa kupata Mikopo ya kuboresha Biashara............ 14
- Ng'ombe wahimilishwa kwenye Kambi Mikoani............ 16
- Ufugaji wa Ngo'mbe unavyoweza kuwa chanzo muhimu cha Nishati............ 19




- Mpina asisitiza Mazingira Bora kwa Wafanyabiashara ya Maziwa Nchini............ 22
- Fahamu faida za Uhawilishaji katika Sekta ya Mifugo............ 23
- Bodi yatakiwa kubuni njia za kuboresha huduma za LITA............ 25
- Maafisa uvuvi watakiwa kusimamia Sheria ili kuongeza pato la Taifa............ 27
- Serikali yapongezwa kwa ulinzi wa Rasilimali Ziwa Victoria............ 29
- Wavuvi waishukuru Serikali kwa kuwapatia Mkopo............ 31
- Kiwanda cha kuchakata Samaki Rukwa chajengwa............ 34
- Wizara kujenga Vituo vya kuzalishia Samaki............ 36
- Dkt. Tamatamah afurahishwa na Sekta Binafsi............ 38
- Mwani, Dagaa kuwekewa Viwango vya Ubora............ 40
- Kituo kikubwa cha Ukuzaji Viumbe Maji kujengwa Chato............ 42
- Ufufuaji wa TAFICO wazidi kupiga hatua............ 44




# MAGUFULI AIPONGEZA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

- ***Asema mauzo ya samaki nje ya nchi yaongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 379 mwaka 2015 hadi bilioni 692 mwaka 2019***
- ***Eneo la ufugaji limeongezwa kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2005 hadi kufikia hekta milioni 5 mwaka 2020***

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa jitihada kubwa ilizozichukua katika kipindi cha miaka mitano ya Uongozi wake ambazo zimesaidia kuboresha na kukuza uchumi wa nchi.

Akizungumza wakati akitoa hotuba yake ya kulifunga Bunge la kumi na moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 16, 2020 jijini Dodoma, Rais Magufuli alisema kuwa katika kipindi hiki cha miaka mitano ya uongozi wake Wizara ya Mifugo na Uvuvi imechukua hatua kadhaa ambazo zimesaidia nchi kufikia mafanikio makubwa.

Rais Magufuli wakati akitaja baadhi ya maeneo ambayo Wizara imeyashughulikia na kupata mafanikio, alisema katika kipindi cha miaka mitano serikali iliongeza eneo la ufugaji kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2005 hadi kufikia hekta milioni 5 mwaka 2020 jambo ambalo amelitaja kuwa limechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli Serikali kupitia Wizara imejenga mabwawa mapya ya kuogeshea ng'ombe 104, imesambaza chanjo na dawa za Mifugo nchi nzima, huku idadi ya ng'ombe waliohimilishwa imeongezeka kutoka laki moja na elfu tano (105,000)



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akizungumza wakati akitoa hotuba yake ya kulifunga Bunge la kumi na moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 16, 2020 jijini Dodoma.

mwaka 2015 hadi kufikia Laki tano kumi na nne elfu na mia saba (514,700).

Aliongeza kuwa Serikali imeimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kuanzisha kanda kuu tatu (3) za Ziwa Victoria, Tanganyika na Pwani ikiwa ni pamoja na kudhibiti zana haramu.

“Nakumbuka kuna wakati nilimuona Mhe. Mpina alikuwa anatembea na rula kwenye Migahawa kupima urefu wa Samaki, hiyo ilikuwa ni katika hatua za kuhakikisha tunapata mafanikio haya ambayo tumeyapata”,alisema Rais Magufuli

Aliendelea kusema kuwa Wizara imehamasisha na kufanikiwa kuongeza idadi ya Wafugaji wa Samaki kutoka laki moja themanini elfu na mia nane arobaini na tatu (180,843) mwaka 2015 hadi kufikia laki mbili sitini elfu mia nne sabini na nne (260,474) mwaka 2020.

“Katika kipindi hiki tumeongeza idadi ya Mabwawa kutoka 220,545 hadi kufikia 260,445 na kuongeza vizimba vya samaki kutoka 109 hadi 431, na uzalishaji wa Vifaranga vya Samaki vimeongezeka kutoka Milioni nane na tisini elfu (8,090,000) hadi Vifaranga Milioni kumi na nne laki tano thelathini na moja elfu, mia nne themanini na saba (14,531,487)”, aliongeza.

Aidha, Rais Magufuli alisema kuwa sambamba na mafanikio hayo serikali imeongezea mtaji kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kiasi cha Shilingi Bilioni Mia Mbili na nane kupitia Mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na kuongeza kuwa Serikali pia imeipatia TADB Dola za Kimarekani Milioni 25 sawa na Shilingi Bilioni 57.8 ili kuendesha Mfuko wa dhamana kwa Wakulima, Wafugaji na Wavuvi.

“Hii ina maana kuwa kwa miaka mitano iliyopita Serikali imeipa TADB Shilingi Bilioni 324.8 kuiwezesha Benki hiyo kutoa mikopo ya moja kwa moja kwa Wakulima, Wafugaji na Wavuvi yenye thamani ya kiasi cha shilingi bilioni 166.9 kwa Riba nafuu”, aliongeza

Kutokana na hatua hizo, Rais Magufuli alisema kuwa mafanikio makubwa yamepatikana ambapo Sangara kwenye ziwa Victoria wameongezeka kutoka tani 417,936 mwaka 2016 hadi kufikia tani 816,964 mwaka 2020.

“Kufuatia hatua hizo, urefu wa Sangara umeongezeka kutoka wastani wa sentimeta 16 hadi kufikia sentimeta 25. 2 jambo ambalo limefanya samaki wetu kuanza kuhitajika kwa kiasi kikubwa katika soko la Ulaya na nyinyi ni mashahidi Waheshimiwa Wabunge Ndege zimeanza kuja Mwanza na kubeba Samaki wetu kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi”, alisisitiza.

Kwa kuzingatia hilo mauzo ya samaki nje ya nchi yameongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 379 mwaka 2015 hadi bilioni 692 mwaka 2019.

Aidha aliongeza kuwa mafanikio hayo sio mambo madogo ni hatua muhimu katika kukuza uchumi wa nchi ambao kwa sasa upo katika hatua nzuri ■




**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akizungumza wakati akitoa hotuba yake ya kulifunga Bunge la kumi na moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 16, 2020 jijini Dodoma.**

# BARAZA KUWAONDOA MADAKTARI FEKI KWENYE SEKTA YA MIFUGO NCHINI

- ***Baraza laandaa beji na vitambulisho kwa ajili ya Madaktari***
- ***Adhabu kali kuwashukia watu watakaokaidi agizo la Baraza***
- ***Baraza lasema lengo ni kulinda taaluma ya udaktari wa mifugo***

Mwanzoni mwa Mwezi Juni, 2020 Baraza la Veterinari lilifanya Mkutano wake wa 45 jijini Dodoma kwa lengo la kufanya tathimini ya kiutendaji ya Baraza hilo.

Pamoja na mambo mengine Baraza hilo liliangazia tasnia nzima ya Udaktari wa Mifugo ambao kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Baraza hilo, Profesa Rudovick Kazwala alisema tasnia hiyo imeingiliwa na watu wasio na sifa na kufanya kazi jambo ambalo limekuwa likichafua taaluma hiyo ya udaktari wa mifugo nchini.

Kufuatia hali hiyo, Baraza la Veterinari limeamua kuandaa Beji na Vitambulisho ambavyo kuanzia mwaka huu vitakuwa vinawatambulisha Madaktari wanaotambulika na Baraza hilo ili kuwaondoa madaktari feki.

Kuonesha kuwa hawafurahishwi na vitendo vya watu hao, Baraza la Veterinari lilitoa tamko la kuwataka watu hao ambao hawana sifa za Udaktari wa Mifugo kuacha mara moja kuhudumia na kutibu mifugo huku likionya kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa watakaao kwenda kinyume na Sheria.




**Mwenyekiti wa Baraza la Veterinari, Profesa Rudovick Kazwala (aliyekaa katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza hilo muda mfupi baada ya kumaliza Mkutano wa 45 wa Baraza la Veterinari ulilofanyika jijini Dodoma Juni 4, 2020. Wa kwanza kulia waliokaa ni Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania, Profesa Hezron Nonga, wa pili ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Veterinari, Dkt. Bhakilana Mafwere. Wa kwanza kushoto waliokaa ni Kaimu RASI wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Afya ya Sayansi ya Jamii – Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Profesa Elliot Phiri, na wa pili ni Msajili wa Baraza la Veterinari, Dkt. Bedan Masuruli.**

"Wale wote wanaojiingiza katika fani hii bila kuwa na vyeti vya kitaaluma wajue kuwa kuna sheria namba 16 ya Veterinari ya mwaka 2003 ambayo inakataza mtu ambaye hajasomea taaluma ya Udaktari wa mifugo kufanya kazi ya kuhudumia na kutibu mifugo, atakayekutwa na kosa hilo sheria itachukua mkondo wake," alisema Profesa Kazwala.

Alisisitiza kuwa kuanzia sasa wafugaji wanapaswa kujua kuwa wataalamu wa mifugo watakuwa na vitambulisho vitakavyokuwa vinatolewa na Baraza hilo na kuwakataa watu watakaokuwa wanakwenda kutaka kutibu mifugo yao bila kitambulisho.

"Huko nyuma hatukuwa na vitambulisho, kukosekana kwa vitambulisho kulisababisha watu wasio na sifa kujiingiza katika kazi ya tiba ya mifugo na kuchafua sifa za fani yetu," alifafanua Profesa.

Kufuatia changamoto hiyo, Profesa Kazwala alisema mkutano huo umekubaliana na kupitisha maamuzi kuwa wataalamu wa mifugo wawe na vitambulisho ambavyo vitasaidia kuzuia na kuwaondoa watu wasio na sifa ya udaktari wa mifugo nchini.

Aliongeza kuwa watahakikisha wakaguzi wa mifugo wanapita kila mara kwa wafugaji kukagua mifugo yao na kufuatilia kama kuna watu kama hao ambao wanaendelea kuvunja sheria.

Profesa Kazwala ametoa wito kwa wafugaji na wananchi kwa ujumla kushirikiana na Baraza hilo kuwakataa watu hao wasio na vitambulisho huku akiwasisitiza hata hao madaktari watakaokuwa na vitambulisho wanapokwenda kutibu mifugo yao kuweka kumbukumbu zao vizuri ikiwemo namba ya usajili ya mtaalamu huyo ili kama likitokea tatizo lolote litakalosababishwa na mtaalamu huyo iwe rahisi kumtambua.

Aidha, Profesa Kazwala amewaeleza wananchi kuwa huduma za mifugo zinaendelea kuboreshwa nchini na kuanzia sasa vituo vyote vinavyotoa matibabu ya wanyama lazima viwe na vifaa vya kuchunguza mifugo kwa maana ya Darubini ili kutoa vipimo sahihi vya Sampuli zitakazokuwa zinachukuliwa kutoka kwa mifugo ■



**Mwenyekiti wa Baraza la Veterinari Tanzania, Prof. Rudovick Kazwala akiongea na waandishi wa habari (hawapo pichani) muda mfupi baada ya kumaliza mkutano wa 45 wa Baraza la Veterinari Tanzania uliofanyika jijini Dodoma.**

# SADC KUTATHMINI ATHARI ZA COVID 19 KATIKA SEKTA ZA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

- ***Waziri Mpina aongoza kikao hicho kwa njia ya mtandao***
- ***Wakubaliana miezi mitatu ya utekelezaji***

Mlipuko wa Maradhi ya Covid 19 ulioikumba Dunia hivi karibuni umewakutanisha Mawaziri wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kujadiliana na kuweka maazimio kadhaa ya kuhakikisha kuwa pamoja na janga hilo sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi haziathiriki kwa kiasi kikubwa.

Katika Mkutano uliofanyika kwa njia ya mtandao (Video Conference) uliohudhuriwa na Mawaziri 11 kati ya 16 na kuongozwa na Mwenyekiti wa Mawaziri hao wa SADC wanaosimamia kilimo, usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, Mhe. Luhaga Joelson Mpina waliazimia kufanya tathmini ya kina kuhusu athari zilizopatikana kutokana na mlipuko wa Maradhi hayo na kukubaliana hatua kadhaa za kuchukua ili kunusuru Sekta hizo.

Akiongea katika Mkutano huo uliofanyika Mei 22,2020 jijini Dar es Salaam, Mhe. Mpina alisema kufuatia mlipuko wa maradhi yanayosababishwa na Virusi vya Corona katika nchi mbalimbali zikiwemo wanachama wa SADC, kikao hicho kiliazimia kupeana miezi mitatu kufanya tathmini ya ugonjwa huo katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi na kutafuta njia za kutatua changamoto zilizosababishwa na ugonjwa huo.

“Tumekubaliana kufanya tathmini na kubaini athari na madhara yaliyojitokeza ya Covid 19 katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, baada ya kubaini athari hizo, nyingine zitatatuliwa ndani ya nchi husika na nyingine kati ya nchi na nchi ambapo tutatafuta suluhu kwa umoja wetu.” Alisema Waziri Mpina.

Aliongeza kuwa mkutano huo umehamasisha na kuweka mikakati ya pamoja kwamba shughuli za ukuzaji viumbe maji zifanywe kwa nguvu kubwa zikiwemo sehemu ambazo hakuna maji ya asili kwa maana ya maziwa, mito na bahari kuhakikisha nao wanafanya shughuli za ufugaji wa viumbe maji.

Akiendelea kutoa majumuisho ya kikao hicho Mhe. Mpina alisema, mawaziri hao wameazimia pia kuweka mikakati ya pamoja ya usalama wa chakula na lishe kutokana na changamoto za ukame, mvua nyingi na wadudu wengi wanaoshambulia mazao ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na lishe bora pamoja na kukabiliana na upungufu wa chakula.

Kuhusu magonjwa yanayovuka mipaka yakiwemo ya mimea, Mawaziri hao wamekubaliana kuweka mikakati ili kuzuia magonjwa hayo na kuifanya Tanzania kama nchi ya kuigwa kwa kuweza kupunguza magonjwa ya




**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Luhaga Mpina (wa nne kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Mkutano wa Mawaziri wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam Mei 22, 2020 kwa njia ya “Video conference” kutathmini athari za mlipuko wa maradhi ya Covid 19 katika sekta za kilimo, Mifugo na Uvuvi.**

mifugo kwa asilimia 29 na kuweza kupunguza vifo vya mifugo kwa asilimia 37.

Aidha, Mhe. Mpina aliongeza kuwa licha ya uwepo wa ugonjwa huo wavuvi wa Tanzania hawajakosa sehemu ya kwenda kuuza samaki na kubainisha namna ndege za mizigo ambazo zimekuwa zikiingia nchini kwa ajili ya kubeba minofu ya samaki kwenda nchi za nje.

“Namna ya kuwasaidia wavuvi ni baada ya kufanya tathmini na kujua mahitaji yao, baadhi ya nchi wamewafungia watu wao na kushindwa kufanya shughuli zao zikiwemo za uvuvi, hivyo tujitathmini katika kipindi cha miezi mitatu namna tutakavyoweza kutoa mchango wetu katika nchi hizo.” Aliongeza Waziri Mpina.

Akifungua Mkutano huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Prof. Elisante Ole Gabriel ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maafisa Waandamizi wa (SADC) aliwaeleza maafisa kutoka Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na maafisa wengine wa nchi wanachama ambao walikuwa katika nchi zao wakifuatilia ufunguzi huo kwa njia ya video kuwa Mwenyekiti wa SADC Dkt. John Magufuli amekuwa akiwahimiza na kuwataka Watanzania na Wanachama wa SADC kuendelea kuchukua tahadhari juu ya ugonjwa wa Covid 19.

Prof. Gabriel aliwaomba maafisa hao wa SADC kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Covid 19 na kuendelea kufanya kazi kwa bidii kama ambavyo Mwenyekiti wa SADC amekuwa akisisitiza kwa wanachama wa SADC.

“Tumelazimika kufanya kikao kwa njia ya video kutokana na changamoto ya Covid 19 na tuweze kushikamana kwa umoja wetu ili kupunguza kasi ya maambukizi, kuchukua tahadhari na kuchapa kazi na kuendelea kumuomba Mungu atusaidie”, alisema Prof. Gabriel

“Tusipotafakari tutaathirika kiuchumi suala ambalo litakuwa gumu zaidi na litaweza kuchukua hata miaka 50 kuweza kukabiliana nalo.”, Aliongeza

Naye, Katibu Mkuu wa SADC Dkt. Stergomena Laurance Tax alisema anafurahishwa na uongozi wa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli kwa namna ambavyo amekuwa akisimamia suala la ugonjwa wa Covid 19.

Dkt. Tax aliendelea kusema kuwa SADC itahakikisha mipango yote ambayo inapangwa na nchi wanachama inatekelezwa kwa faida ya jumuiya hiyo ili iwe endelevu.

Kikao hicho cha Mawaziri wa SADC wanaosimamia kilimo, usalama wa chakula, mifugo na uvuvi kilihudhuriwa na mawaziri kutoka nchi 11 kati ya 16 ambazo ni Angola, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Eswathini.

Nchi Nyingine ni Malawi, Msumbiji, Namibia, Seychelles, Afrika Kusini, Tanzania, Zambia na Zimbabwe.

Agosti 17, 2019 Tanzania ilikabidhiwa Uenyekiti wa SADC kutoka kwa nchi ya Namibia ■




**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Luhaga Mpina(kulia) akifurahia jambo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel (kushoto) katika kikao cha Mawaziri wa SADC kilichofanyika jijini Dar es Salaam kwa njia ya video conference kutathmini athari za mlipuko wa maradhi ya Korona katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi Mei 22, 2020.**

# WIZARA YAJIPANGA KUTOKOMEZA MAGONJWA YANAYOATHIRI MIFUGO

- ***Yazalisha chanjo 6 kati ya 13 ilizopanga kuzalisha.***
- ***Yajenga majosho 101 na kukarabati 578.***
- ***Yashusha bei ya chanjo ya homa ya mapafu kufikia shs. 550 kwa dozi.***

Miongoni mwa changamoto ambazo zimekuwa zinasumbua Sekta ya Mifugo ni magonjwa yanayoiandama mifugo ambapo kwa kiasi kikubwa magonjwa hayo yamechangia kuzorotesha uzalishaji wenye tija unaotokana na mifugo nchini.

Kwa Mujibu wa maelezo ya Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Tanzania, Profesa Hezron Nonga, magonjwa ambayo wameyapa kipaumbele kuyadhibiti ni kumi na tatu (13) na kati ya hayo magonjwa, mdudu Kupe peke yake anachangia vifo vya Ng'ombe husussan ndama kwa zaidi ya asilimia 70.

"Pamoja na Tanzania kuwa na mifugo isiyopungua milioni 34 bado wingi huo wa mifugo haujaleta tija kubwa ya uzalishaji kama inavyotarajiwa na hii ni kutokana na magonjwa yanayoandama mifugo hiyo", alisema Profesa Nonga

Kutokana na hali hiyo, Mwaka 2018 Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliamua kuja na mkakati wa kufanya mageuzi makubwa katika huduma za mifugo upande wa afya ili kuwa na mifugo bora itakayotoa mazao bora na salama kwa matumizi ya binadamu.

Mkakati huo ambao umejikita zaidi katika kukinga mifugo dhidi ya magonjwa, umeweka utaratibu wa kuhakikisha mifugo yote inaogeshwa na kupata chanjo stahiki dhidi ya magonjwa ya kipaumbele.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo magonjwa yanayochangia kukwamisha uzalishaji wenye tija kwa ng'ombe nchini ni ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya ng'ombe, Miguu na Midomo, NdiganaKali na Mapele ngozi.

"Lengo letu ni kuhakikisha mifugo yote nchini inapata chanjo kulingana na kalenda ya uchanjaji ili kuwakinga na magonjwa hayo sumbufu", alisema Profesa Nonga

Ili kuhakikisha chanjo zinapatikana kirahisi Serikali kupiti Wizara imeweka utaratibu mzuri wa ununuzi wa pamoja wa chanjo (bulk procurement system) na zitasambazwa katika maeneo yote kuanzia ngazi ya kijiji mpaka ngazi



**Serikali ya awamu ya tano imeendelea kuboresha miundombinu ya sekta ya mifugo nchini kwa kujenga na kuikarabati iliyopo. Hili ni mojawapo ya josho lililojengwa mkoani Simiyu ambalo hutumika kuogesha mifugo ili kuikinga na maradhi hususan maradhi yaenezwayo na kupe.**

ya mkoa ili ziwe zinapatikana kwa urahisi.

“Utaratibu huu wa ununuzi wa pamoja unatarajiwa kuanza kufanya kazi mwezi Oktoba mwaka huu ambapo chanjo zote za Kipaumbele zitapatikana kuanzia ngazi ya kijiji mpaka mkoani”, alisisitiza

Akifafanua hoja ya baadhi ya wafugaji wanaolalamika kuwa chanjo zimekuwa zikiuzwa kwa bei kubwa, Alisema kuwa chanjo ni huduma sio biashara na ndio maana serikali katika mkakati huu imeweka bei elekezi ya chanjo hizo ili kila mfugaji aweze kununua, huku akitolea mfano bei ya chanjo ya homa ya mapafu ya ng’ombe ambayo ni shilingi 550.

“Nia ya Serikali ni kumsaidia mfugaji kuwa na mifugo yenye afya bora ambayo itatoa mazao bora na salama kwa mtumiaji, unaweza kuona kwa mfano Ng’ombe mwenye gharama kubwa Serikali imefanya chanjo yake ipatikane kwa shilingi 550 tu, hivyo ni matarajio yetu wafugaji watachangamkia fursa hiyo”, alifafanua



**Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Dkt. Furaha Mramba akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wakala hiyo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya chanjo iliyofanyika katika Wilaya ya Mkalama Mkoani Singida hivi karibuni.**

Aidha, Serikali imetunga Kanuni ya Chanjo na Uchanjaji ya mwaka 2020 inayomlazimisha mfugaji kuchanja mifugo yake dhidi ya magonjwa ya kipaumbele. Pia, kanuni ya chanjo na ununuzi wa chanjo kwa pamoja utasaidia upatikanaji wa chanjo kwa wakati na kanuni itasaidia kuelekeza ratiba ya uchanjaji kwa mwaka mzima.

Mkakati huo umepanga kuwa katika kila Kijiji, Kata, Wilaya hadi Mkoa kuwe na Majosho ya kuogeshea ng’ombe na mifugo mingine walau mara mbili kwa mwezi ili kuwalinda na maradhi yanayosababishwa na Kupe pamoja na wadudu wengine.

Katika kuhakikisha suala la kuogesha mifugo linafanikiwa kwa mwaka huu wa fedha wa 2019/2020 Serikali imeshajenga majosho 101 na kukarabati majosho 518 na kusisitiza lengo likiwa kuwakinga mifugo na vifo vinavyosababishwa na magonjwa hayo.

Katika hatua nyingine Profesa Nonga alisema suala la uogeshaji wa mifugo ni la lazima, Serikali imetunga Kanuni ya uogeshaji na matumizi ya dawa za kuogeshea ya mwaka 2020 ambayo inawataka wafugaji kuogesha mifugo yao.

“Kanuni hii inamlazimisha mfugaji kuogesha mifugo yake walau mara mbili kwa mwezi kinyume na hapo ni kosa na adhabu yake ni kulipa kiasi cha shilingi milioni kumi kama faini au jela mwaka mmoja au vyote kwa pamoja kutegemeana na kosa lenyewe” alisisitiza Profesa Nonga

Alisema kuwa Serikali inanunua dawa na kuzigawa bure katika majosho na mfugaji atachangia shilingi hamsini (50) tu kwa kila mchovyo mmoja kwa ng’ombe na shilingi kumi (10) kwa Mbuzi na Kondoo ikiwa ni kama mchango wa uendeshaji.

Alitoa wito kwa wafugaji wote kwenda sambamba na kasi ya Serikali ya awamu ya tano kwa kuhakikisha wanakuwa na mifugo bora itakayozalisha malighafi zitakazoenda viwandani kwa wingi na kwa ubora unaohitajika ili kukuza uchumi wa viwanda.

Akizungumzia chanjo ambazo zimeshazalishwa mpaka sasa, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Prof. Hezron Nonga alisema kuwa mpaka sasa Wizara imeshazalisha takriban chanjo aina sita (6) kati ya chanjo kumi na tatu (13) ambazo wanataka kuzizalisha.

Changamoto iliyopo anasema ni uwepo wa watu ambao wanajihusisha utoaji wa chanjo usiozingatia weledi lakini watambue sheria ipo na inakataza mtu asiye daktari wa mifugo kujishughulisha na utoaji wa huduma za chanjo kwa mifugo ■

# WAZALISHAJI WA MAZIWA WAHIMIZWA KUTUMIA MASOKO RASMI

- ***Takwimu zinaonesha kuwa Asilimia tisini (90%) ya maziwa yote yanauzwa katika soko lisilo rasmi***

Dunia ikiwemo Tanzania huadhimisha wiki ya Maziwa kila ifikapo Mei 28 hadi Juni 1 ya kila mwaka huku lengo kuu likiwa ni kuhamasisha unywaji wa maziwa salama kwa wingi ili kujenga afya ya jamii na kuchochea soko la bidhaa hiyo.

Nchini Tanzania,Maadhimisho hayo hufanyika katika maeneo ya wazi hasa viwanjani ili kuhakikisha wadau mbalimbali wa tasnia ya maziwa wanapata fursa ya kuonesha aina na matumizi sahihi ya bidhaa walizonazo na kivutio kikubwa huwa ni mashindano ya unywaji wa maziwa ambayo sehemu kubwa hutumika kuionesha jamii ni kiasi gani maziwa ni chakula muhimu kwa mahitaji ya mwili wa binadamu.

Uwepo wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona ulisababisha maadhimisho ya Wiki ya maziwa kwa mwaka 2020 yafanyike kwa njia kutumia vyomboa vya habari ambapo wananchi walipata fursa ya kushuhudia jitihada mbalimbali za wadau wa tasnia ya maziwa kupitia makala za uzalishaji na usindikaji zilizoangazia wadau mbalimbali wa tasnia ya maziwa kutoka kanda za kusini na kaskazini mwa Tanzania.

Mbali na Makala hizo, maadhimisho hayo yalipambwa na vipindi mbalimbali vya redio, televisheni na makala zilizochapishwa kwenye magazeti mbalimbali huku maudhui ya vyombo vyote hivyo yakiwa ni namna ya kuiboresha tasnia ya maziwa na kuongeza kiwango




**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina, akinywa maziwa akiwa pamoja na viongozi na wadau wa maziwa katika mojawapo ya siku ya maadhimisho ya wiki ya unywaji wa maziwa duniani.**

cha unywaji wa maziwa nchini ambacho mpaka sasa kinakadiriwa kufikia lita 49 tu kwa mwaka huku lengo likiwa ni kufikia lita 200.

Pia Maadhimisho hayo yaliambatana na zoezi la ugawaji wa maziwa kwenye vituo vya watoto yatima na vituo vya kutolea huduma za afya ambapo jumla ya lita 1,650 za maziwa, barakoa 1000 na ndoo 15 za maji tiririka ziligawiwa katika vituo vinne (4) ambavyo ni Kituo cha Watoto yatima cha Kisedeti, Kijiji cha Matumaini, Kituo cha Afya cha Mkonze na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma.

Aidha jumla ya lita 1,743 ziligawiwa kwa watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na katika mikutano mbalimbali ya wadau huku lita nyingine 2,064 za maziwa zikitolewa Mkoani Dar es Saalam katika vituo 36 vya Watoto yatima.

Katika hotuba yake ya uzinduzi wa Wiki ya Maziwa 2020,jijini Dodoma, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mhe. Abdallah Ulega alitoa hamasa kwa wananchi kunywa maziwa kwa wingi kadri inavyowezekana huku rai kubwa akiielekeza kwa wasindikaji wa maziwa nchini kuwa na mshikamano ili kuzitumia vema fursa zilizopo kwenye tasnia ya maziwa.

“Najua mnafanya biashara na kwenye biashara ushindani ni lazima lakini ningependa ushindani wenu ulenge fursa zilizopo ili mzalishe maziwa na bidhaa zake kwa wingi na hatimaye mkidhi mahitaji ya soko” Alisema.

Katika kuhakikisha desturi ya unywaji maziwa nchini inaendelezwa kwa watu wa rika tofauti, Bodi ya Maziwa hufanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuratibu mpango maalum wa unywaji maziwa kwa wanafunzi wa shule za Msingi ambapo mpaka sasa mpango huo unatekelezwa katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Njombe,Iringa na Dar-es-salaam ambapo jumla ya wanafunzi 34,561 kutoka zaidi ya shule 40 wamenufaika na mpango huo kwa kunywa zaidi ya lita 631, 860.

Hata hivyo pamoja na jitihada hizo za dhati zinazofanywa na Serikali bado kiwango cha unywaji wa maziwa yanayozalishwa nchini kipo chini na moja ya sababu zilizotajwa kusababisha hali hiyo ni dhana ya Watanzania kupendelea zaidi bidhaa za maziwa zinazozalishwa nje ya nchi.

Aliyekuwa Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa Dkt. Sophia Mlote alikiri kuwepo kwa changamoto hiyo ambapo alielezea jitihada kadhaa ambazo zimekuwa zikifanywa na bodi yake katika kutatua changamoto hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa unywaji wa maziwa salama.

“Lakini pia katika kuhakikisha tunalinda afya za walaji pindi wanapokunywa maziwa, serikali imetunga sheria ambayo inasimamia mazingira ya usafirishaji na uhifadhi wa maziwa ambayo inazuia maziwa kuhifadhiwa kwenye vyombo vya plastiki na kusafirishwa kwenye gari lenye mizigo ambayo si chakula” aliongeza.

Hata hivyo badala ya kufunga maadhimisho hayo Juni mosi, ulifanyika mjadala mpana jijini Dodoma na kurushwa mubashara na TBC, lengo likiwa ni kufahamu na kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili wadau mbalimbali wa tasnia ya maziwa ili kuzidi kuifanya tasnia hiyo kuendelea zaidi na kufikia lengo la uzalishaji wa maziwa ambalo ni lita bilioni 7 kufikia 2025.

Mjadala huo uliokuwa na mada isemayo “Nini kifanyike kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa nchini”uliongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia sekta ya mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel na kujumisha viongozi na watendaji mbalimbali wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Umoja wa wazalishaji wa maziwa nchini (TAMPRODA), Umoja wa wasindikaji wa maziwa nchini (TAMPA), wafugaji na wazalishaji wadogo wa maziwa na wananchi ambao walishiriki mjadala huo kwa njia ya televisheni kwa kupiga simu na kutoa hoja zao moja kwa moja.

Kwenye hotuba yake ya kuhitimisha mjadala huo, Prof. Ole Gabriel alisema kuwa ni wakati sasa umefika kwa wananchi kuanza kuthamini bidhaa za maziwa zinazozalishwa hapa nchini ili kuwaongezea nguvu wazalishaji wa ndani.

“Tunaweza kuwa tunajadili ni namna gani tunaweza kuongeza kiwango cha unywaji wa maziwa, kumbe wanywaji ni wengi lakini wanatumia zaidi bidhaa za nje hivyo nitoe rai kwa Watanzania tutumie zaidi bidhaa zetu ili kuwaongezea nguvu na ari wazalishaji wetu wa ndani” Alisisitiza.

Baadhi ya maazimio yaliyoibuliwa kwenye mjadala huo ni pamoja na lile lililotaka wafugaji waelimishwe ili wafuge kibiashara na watambue kuwa ufugaji ni ajira na waipende mifugo yao , uimarishaji wa miundombinu wezeshi ya kuwasaidia wazalishaji wa maziwa kupata soko la uhakika kwa kuendeleza mpango maalum wa unywaji wa maziwa shuleni, kuwa na kampeni endelevu za pamoja kati ya sekta binafsi na serikali kuhusu unywaji wa maziwa huku pia Serikali ikitakiwa kuweka ruzuku kwenye pembejeo na vifaa vya usindikaji wa maziwa.

Katika taarifa yake aliyoisoma siku ya kilele cha wiki

ya maziwa kilichofanyika kwenye ukumbi wa Mkapa Mwakilishi wa Chama cha Wazalishaji wa Maziwa Tanzania (TAMPRODA), Bi. Suzan Majala aliishukuru Serikali kwa kuwasaidia wafugaji nchini kuwaondolea changamoto kubwa katika ufugaji na uzalishaji wa maziwa nchini ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa chanjo bora za magonjwa ya mifugo kama homa ya mapafu, Ndigana kali, ugonjwa wa midomo na miguu.

Aidha, alieleza kuwa Wizara imesaidia kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji kwa kutenga maeneo maalumu ya kufugia, kupata huduma za uhimilishaji kwa gharama nafuu, kujenga majosho ya kuogeshea mifugo, upatikanaji wa madawa ya kuogeshea mifugo kwa gharama nafuu na upatikanaji wa mikopo ya ng'ombe wa maziwa kwa masharti nafuu.

Katika hotuba yake ya kuhitimisha maadhimisho ya Wiki ya Maziwa Mwaka 2020 jijini Dodoma, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina alitoa wito kwa wananchi, taasisi binafsi na za Serikali kutumia maziwa yanayozalishwa nchini badala ya kuagiza kutoka nje huku akisisitiza kuendelea kuongeza kodi kwa maziwa yatakayokuwa yakiingia kutoka nje.

Mhe. Mpina aliwasisitiza Wasindikaji na Wamiliki wa Viwanda kusindika maziwa kulingana na uwezo wa viwanda (Installed capacity) kuliko ilivyo sasa ambapo wanasindika asilimia 23.52 tu ya uwezo wao jambo linalosababisha maziwa mengi kumwagwa kwa kukosa soko na kusababisha maziwa mengi kutokusindikwa na hali hivyo kusababisha ongezeko la utegemezi wa maziwa kutoka nje ya nchi.

“Lengo la Serikali ni kuhakikisha ndani ya kipindi cha miaka mwili ijayo nchi haiagizi tena maziwa kutoka nje na katika kuhakikisha mpango huo unakamilika, inakusudia kujenga viwanda vikubwa vitano vya kusindika maziwa katika mikoa ya Mbeya, Kagera, Mara, Mwanza na Shinyanga hivyo ninatoa wito kwa wadau na viongozi wa Mikoa husika kutoa ushirikiano unaostahili ili kufikia malengo hayo ya Serikali” Alihitimisha ■



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akinywa maziwa katika mojawapo ya siku ya maadhimisho ya wiki ya unywaji wa maziwa duniani.**

# KAMPENI ONDOA MAGOGO KWENYE MABUCHA NI ENDELEVU: MSAJILI WA BODI

- ***Takwimu zinaonesha mpaka sasa ni asilimia hamsini (50%) ya wafanyabiashara wa nyama wanatumia mashine za kisasa.***
- ***Walaji washauriwa kutonunua nyama kwenye bucha zinayotumia magogo.***
- ***Wafanyabiashara wakumbushwa kuzingatia maelekezo ya Bodi ili kuepukana na adhabu.***

Mwaka 2009 Bodi ya Nyama Tanzania ilianzisha Kampeni ya ondoa magogo kwenye Bucha na kuhamasisha matumizi ya mashine za kukatia nyama kwa lengo la kuwaepusha walaji na madhara yanayoweza kupatikana kutokana na matumizi ya magogo hayo.

Kampeni hiyo ilianzishwa kufuatia maelekezo ya Waziri Mkuu (Mst), Mheshimiwa Mizengo Pinda yaliyotaka kufanyika uboreshaji wa Bucha ili ziwe za kisasa kwa kutumia vyombo stahiki.

Kwa Mujibu wa Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichalwe, toka zoezi hilo lianze mpaka sasa takwimu zinaonesha ni asilimia hamsini (50%) ya Wafanyabiashara wa Bucha za nyama wamezingatia maelekezo na wameanza kutumia mashine hizo.

Akitoa sababu za kuanzisha kampeni hiyo alisema, utumiaji wa magogo katika Bucha sio salama kwa afya ya mlaji kwa sababu magogo yanatunza uchafu ambao unasababisha wadudu kuzaliana kwa wingi na ikitokea nyama iliyoathiriwa na wadudu hao kuliwa bila kuchemshwa au kuchomwa vizuri, mlaji anaweza kudhurika kwa kupata magonjwa ya tumbo yakiwemo yale ya kuhara.

"Matumizi ya magogo sio salama kwa sababu yanatunza uchafu unaosababisha wadudu kuzaliana na hivyo kuweza kuhatarisha afya za walaji na kushusha ari ya ulaji wa nyama ambao unaathiri biashara," alisema Bw. Imani.



**kipande cha gogo la mti kama kilivyokutwa hivi karibuni kikitumika kukatia nyama katika moja ya Bucha jijini Dodoma.**

Akizungumzia kuhusu mikakati waliyonayo kuhakikisha matumizi ya magogo yanakwisha katika Bucha, Sichalwe alisema, Bodi ya nyama itaendelea na kampeni hii kwa kutoa elimu kwa jamii na wafanyabiashara hao kupitia vyombo vya habari ili kuwajengea uelewa juu ya umuhimu wa kutumia mashine hizo.

"Tunaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaokaidi maelekezo ya Bodi," alisema.

Aliongeza kuwa Bodi ya nyama imekuwa ikiwaelimisha wafanyabiashara kuacha kutumia magogo na badala yake watumie mashine kwa sababu faida za mashine ni pamoja na usafi kwa afya ya mlaji.

"Mashine za kukatia nyama zinapatikana katika maduka yanayojishughulisha na uuzaji wa vifaa vinavyotumika katika maduka ya nyama au Bucha. Maduka haya yamesambaa nchi nzima ikiwa ni pamoja na nchi jirani za Kenya na nyinginezo," alisisitiza.

Akieleza kuhusu changamoto wanazokabiliana nazo katika zoezi hilo, Sichalwe alisema changamoto kubwa ni ukaidi wa maagizo ya serikali, kuna baadhi ya wafanyabiashara hawazingatii maelekezo yaliyotolewa.

Pia, alisema changamoto nyingine wanayoipata ni walaji kuendelea kununua nyama katika Bucha zinazotumia magogo aidha kwa kutokufahamu au kwa sababu wengi wao kutosikiliza elimu ya biashara ya nyama na ulaji ambayo inatolewa mara kwa mara kwenye vyombo vya habari.

Christopher Mwakabana, muuzaji wa Bucha la Jumba la Dhahabu jijini Dodoma anasema zoezi hilo la kuondoa magogo wamelipokea kwa mikono miwili na kimsingi mashine ya kukatia nyama ina faida nyingi katika kuwahudumia wateja maana inafanya nyama iwe na muonekano mzuri ukilinganisha na nyama iliyokatwa bila mashine.

"Mashine inatusaidia tusitumie nguvu kazi nyingi wakati wa ukataji wa nyama na hata mifupa, pia inapunguza upotevu wa nyama ukilinganisha na ukitumia gogo," alisema

Aliendelea kusema kuwa utumiaji wa mashine unawawezesha kupata wateja wakubwa kama wamiliki wa Mahoteli, Migahawa mikubwa na Wateja wengine wenye hadhi ambao wanapendelea kununua nyama kwenye Bucha ambazo ni safi na zinazotumia mashine.

Akieleza kuhusu changamoto anasema mashine hizo zinaambatana na gharama za mara kwa mara ambazo mfanyabiashara lazima atazipata ikiwemo kununua vifaa vingine vya kusapoti kama Mkanda, msumeno ambavyo vinatakiwa kubadilishwa mara kwa mara kwa sababu ya kuisha au kushika kutu.

Aliongeza kuwa mashine hizo upatikanaji wake bado ni mgumu hususani kwa walio mikoani, maana ukiwa mkoani na unataka kuanza biashara unatakiwa kuagiza mashine kutoka Dar es Salaam hivyo inakuwa ni gharama kubwa.

"Ukitaka kutumia mashine ni lazima uwe na umeme wa uhakika maana kama umeme utakatika ina maana hauwezi kufanya biashara, mashine hizi pia zinahitaji ujuzi hivyo mafunzo ni muhimu bila hivyo ni rahisi sana kuziharibu,"alisema.

Christopher ameongeza kuwa ili zoezi la kampeni ondoa magogo lifanikiwe inabidi serikali itafute mbadala wa magogo kwa wingi, kwa mfano serikali ilianzisha vibao vya plastiki kama mbadala wa magogo lakini bado upatikanaji wake ni adimu sana.

Aidha, Christopher aliishauri serikali kuhakikisha inaweka bei nafuu za mashine hizo na izisambaze katika mikoa yote ili iwe rahisi kupatikana.

Mteja wa nyama katika Bucha la Jumba la Dhahabu, Bi. Starhailat Habibu anasema yeye anapendelea kununua nyama ambayo inakatwa kwa kutumia mashine maana inakua safi na pia inafanya nyama iwe na muonekano mzuri.

Josephat Mwasope, mmoja wa wauzaji wa nyama, Mkoani Dodoma, anasema kuwa bado anatumia magogo kwasababu mashine zinapatikana kwa gharama kubwa ukilinganisha na mtaji wake.

Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichalwe anatoa wito kwa wadau wote kufuata maelekezo ya Bodi ili kuepukana na adhabu na kuwaepusha walaji na madhara yanayoweza kuwapata huku akiwataka walaji kuacha kununua nyama katika Bucha zinazotumia magogo au zinazouza katika mazingira ya uchafu mwingi ■




**Baadhi ya bucha pamoja na kununua mashine za kukatia nyama bado zinaendelea pia kutumia magogo kama inavyooneka katika picha. Muuzaji akiwa ameshika kipande cha gogo wakati ndani kuna mashine ya kukatia nyama.**

# WAFUGAJI NA WAVUVI WAWEZESHWA KUPATA MIKOPO YA KUBORESHA BIASHARA

** Ni ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 17.3 zilizotolewa mwaka 2018/2019*

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa Wafugaji na Wavuvi wanawezeshwa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilianzisha Dawati la Sekta Binafsi kwa lengo la kuwa kiungo kati ya serikali na sekta binafsi kwa kuratibu na kufuatilia uwekezaji kwenye sekta ya mifugo na uvuvi.

Pia, kuweka mifumo mizuri ya kuwatambua wafugaji na wavuvi, kujua changamoto zao za kodi na zisizo za kikodi ili kuzitatua ikiwemo kuwaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupata mikopo na huduma nyingine za fedha.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Dawati la Sekta Binafsi, Stephen Michael kwa mwaka fedha wa 2019/2020 Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kupitia Dawati hilo iliidhinisha shilingi bilioni 26.1 kwa ajili ya utoaji mikopo kwenye vyama vya ushirika vya wafugaji na wavuvi, makampuni na mkopaji mmoja mmoja.

Alisema kuwa mkopo huo ni ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 17.3 zilizotolewa mwaka 2018/2019.

Michael anasema kabla ya Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Magufuli haikuwa rahisi kwa taasisi za kifedha kutoa mikopo kwa wafugaji na wavuvi kwa kuwa iliaminika kuwa hawana dhamana kutokana na shughuli wanazofanya.

"Kupitia vyama vya ushirika, Dawati limeweza kuwaunganisha wafugaji na wavuvi na taasisi za kifedha hususan Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ili waweze kupata mikopo", alisema.

Anasema kwa msingi huo, Serikali ya awamu ya tano imeweka mipango ya kuhakikisha kuwa wafugaji na wavuvi wanafanya uwekezaji utakaochangia malighafi kwa ajili ya kuelekea kwenye mapinduzi ya viwanda




**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akionesha mfano wa hundi wakati akikabidhi mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa Chama cha Ushirika wa Wavuvi Bukasiga kilichopo Wilayani Ukerewe, Mkoani Mwanza hivi karibuni.**

ambayo malighafi nyingi inatokana na sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Anaongeza kuwa ili kufikia malengo hayo ya serikali, Wizara inafanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya ufugaji wa kibiashara, kuwahamasisha wafugaji na wavuvi kujiunga pamoja.

Jitihada nyingine ni Serikali kuwahamasisha wafugaji na wavuvi kuanzisha vyama vya ushirika ambavyo vitawarahisishia kupata mikopo kwa urahisi ukilinganisha na mfugaji mmoja mmoja.

Michael anasema moja ya changamoto kubwa waliyonayo wadau wa sekta ya mifugo na uvuvi ni mitaji na dhamana. Ukosefu wa mitaji na dhamana umesababisha baadhi ya wadau kushindwa kununua zana bora za kuzalishia pamoja na kushindwa kufanya uwekezaji wa kiushindani na wenye faida, serikali kwa kuliona hilo iliamua Dawati la Sekta binafsi na Benki ya TADB kuwawezesha wafugaji na wavuvi hao kupata mikopo hiyo kupitia vikundi vyao.

“Kwa makampuni na mkopaji mmoja mmoja benki ya TADB imeidhinisha jumla ya mikopo ya shilingi bilioni 25.2 kwa sekta ya mifugo na milioni 944.2 kwa sekta ya uvuvi” alisema.

“kwa mikopo ya vyama vya ushirika, benki ya TADB imeidhinisha mkopo wa shilingi milioni 146 kwa vyama vya ushirika vya msingi viwili (2) vya CHAWAMU kilichopata mkopo wa shilingi 100,407,000 na UWAMWA kilichopata mkopo wa shilingi 45,530,000”, aliongeza.

Michael alilisitiza kuwa mikopo hiyo ni utekelezaji wa dhana ya kuwawezesha wafugaji kupitia vikundi au ushirika kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015 – 2020.

Mfugaji wa ng’ombe wa Wilayani Muheza, Mkoani Tanga, Hamidu Semema ameishukuru Serikali ya awamu ya tano kwa kuwasaidia kupata mikopo iliyowasaidia kupata ng’ombe bora na kujenga mabanda ya kisasa.

“Sisi wafugaji baadhi yetu tusingeweza kumudu gharama za kununua hawa ng’ombe, hivyo naishukuru serikali kwa kutusaidia kupata mkopo huu. Pia ni nawashauri wafugaji wenzangu kujiunga na vyama vya ushirika kwani kupitia umoja huu tutaweza kupata mkopo pamoja na mafunzo mbali mbali,” alisema Semema.

Kwa upande wa vyama vya ushirika vya wavuvi, Michael amesema kupitia Dawati chama cha ushirika cha BUKASIGA kilichopo wilaya ya Ukerewe, Mwanza kimepata shilingi milioni 200 wakati chama cha ushirika cha ZILAGULA kilichopo halmashauri ya Buchosa, Wilayani Sengerema kimepata shilingi milioni 100.7 ikiwa ni jumla ya shilingi milioni 300.7 kutoka TADB.

“Hii ni fursa kubwa kwa wavuvi kwa kuwa katika kipindi kirefu wavuvi walikuwa na changamoto ya kutokuaminika na kupata ugumu wa kupata mikopo katika taasisi za kifedha kutokana na shughuli zao kuonekana za kuhama hama na kukosa dhamana”, alifafanua.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika ZILAGULA, Joram Yuda amesema wanaishukuru serikali kwa kuwa sasa wanaaminika na taasisi za kifedha na kupatiwa mikopo ambayo inawasaidia kujiendeleza katika sekta hiyo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika BUKASIGA, Jambula Lugola pamoja na kuishukuru serikali anasema kupitia mkopo huo shughuli zao za uvuvi zitabadilika kwani sasa wataweza kufanya uvuvi wa kisasa zaidi.

“Mkopo huu wa ng’ombe na banda la kufugia tulioupata kutoka benki ya TADB umekuwa na manufaa kwetu kwa kuwa sasa nafuga ng’ombe wawili ambao wananipatia maziwa mengi, kwa siku kila ng’ombe ananipatia maziwa lita 15, ng’ombe hawa wanaozalisha kwa tija wanatuwezesha kulipa mkopo huu kwa muda mfupi zaidi”, anasema Beatrice Mselemu, mfugaji wa ng’ombe kutoka Wilaya ya Muheza, Tanga.

Wakati akikabidhi mikopo hiyo kwa vyama vya ushirika, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega aliwataka wanachama wa vyama hivyo pamoja na viongozi wao kuhakikisha wanaitumia mikopo hiyo kwa malengo yaliyokusudiwa.

“Lengo la Serikali ni kuhakikisha wavuvi na wafugaji mnaongeza kipato kwa kuyaongezea thamani mazao mnayopata. Hivyo kupitia mikopo kutoka benki ya TADB tatizo la mitaji lililokuwa ni kikwazo kwenu litakuwa limetatuliwa”, alisema Ulega.

Mratibu wa Dawati la Sekta Binafsi, Stephen Michael amesema katika kipindi hicho hicho, Benki ya Posta ya Tanzania (TPB) imefungua dirisha maalum la mikopo kwa wavuvi, mfumo wa taarifa za vyama vya ushirika vya wavuvi (Uvuvi Data Base), ambapo vyama vya ushirika 9 na wavuvi 557 kutoka mikoa ya Mwanza, Geita na Kigoma wameingizwa katika mfumo huo utakaowezesha taasisi za fedha kuwatambua na kuwafuatilia wakopaji, hivyo kuvutia utoaji wa mikopo kwa wavuvi.

Aidha, alisema kuwa Dawati hilo limeendelea kufanya kazi karibu na taasisi za kifedha ikiwemo, NMB, CRDB, NBC na TPB ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwenye sekta za mifugo na uvuvi. Pia, Dawati linafanya kazi na taasisi zisizo za kifedha zinazotoa michango mbalimbali ya kisera, mafunzo, tafiti na utaalamu kama vile ANSAF, DALBERG, ASPIRES, SAGCOT na Heifer International-TMPP ■

# NG'OMBE WAHIMILISHWA KWENYE KAMBI MIKOANI

Teknolojia ya Uhimilishaji ni njia ya kisayansi ambayo kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikiwahamasisha wafugaji kuitumia ili kuboresha kosaafu za mifugo yao.

Katika jitihada za kuhamasisha wafugaji kutumia njia hiyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanzisha Kambi za uhimilishaji ambazo zinahusisha mkusanyiko wa wataalam wa uhimilishaji kutoka ngazi ya Wizara, Mikoa na Wilaya katika eneo moja kwa lengo la kutoa huduma ya uhimilishaji kwa wafugaji na kubadilishana utaalamu kuhusiana na teknolojia hiyo.

Toka zoezi hilo la kambi za uhimilishaji lianzishwe tayari ng'ombe 6,255 wamehimilishwa katika mikoa ya Katavi, Simiyu, Dodoma, Kagera,Geita na Pwani.

Kupitia Kambi hizo za uhimilishaji wafugaji 1,173 wamepatiwa elimu katika Wilaya za Kongwa, Mpanda,Bariadi, Meatu, Chato, Bukombe, Misenyi, Kyerwa, Mkuranga, Bunda na Butiama ikiwemo kuwajengea uwezo wahimilishaji na kutoa vifaa vya uhimilishaji bure kwa ng'ombe wote waliohimilishwa katika kambi hizo.

Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti na Mafunzo, Dkt.Hassan Mruttu anasema mafanikio yaliyopatikana toka kuanza kambi za uhimilishaji ni pamoja na kutoa elimu ya uhimilishaji kwa wafugaji 1173 katika Wilaya za Kongwa, Mpanda,Bariadi, Meatu, Chato, Bukombe, Misenyi, Kyerwa, Mkuranga, Bunda na Butiama, kuwajengea uwezo wahimilishaji na kutoa vifaa vya uhimilishaji bure kwa ng'ombe wote waliohimilishwa katika kambi hizo.

Hata hivyo, Dkt. Mruttu anasema pamoja na mafanikio hayo, kumekuwa na changamoto mbalimbali katika zoezi hilo ikiwa ni pamoja na wafugaji kutokuwa tayari kuhimilisha mifugo yao kwa sababu ya kuwa na elimu duni ya zoezi hilo na kutopatikana kwa rasilimali fedha kwa wakati.

Anaongeza kuwa ubovu wa miundombinu ulichangia baadhi ya maeneo kutofikika kutokana na kuharibika kwa barabara kutokana na mvua kubwa zilizokuwa zikiendelea.

Changamoto nyingine ni baadhi ya wafugaji kutofuata masharti ya utunzaji ng'ombe baada ya kutambuliwa



**Afisa Mifugo kutoka kituo cha Uhimilishaji NAIC Bw. Juma Mohammed akikagua ng'ombe kwa ajili ya maandalizi ya uhimilishaji kwenye kijiji cha Kondomwelanzi Wilaya ya Mkuranga Mkoani Pwani hivi karibuni.**

na kuchomwa sindano za kuchochea joto.

Anasema Dkt.Mruttu kuwa wafugaji wametoa ushirikiano wakati wa zoezi hilo kwa kuweza kutenga mifugo yao kwa muda wa mwezi mmoja kwa ajili ya kuhimilishwa na limekuwa na faida kwao kwa kupata mifugo mingi kwa wakati mmoja, Uhitaji wa mbegu za majike kwa mifugo imeongezeka sana kwani wafugaji wengine wamekosa mbegu za ruzuku na kuwa tayari kununua mbegu.

“Wafugaji wameitikia sana zoezi hili la kuhimilisha mifugo yao kiasi kwamba kupelekea mbegu za ruzuku kuisha kwa haraka hata watu wengine kukosa kabisa, hivyo kuna haja ya kujipanga na kuongeza mbegu nyingi zaidi, baadhi ya maeneo kama Meatu na Bariadi wafugaji wameleta maombi ya kufanyika kwa kambi nyingine za uhimilishaji katika maeneo yao ili ziweze kuwahudumia,”anasema.

“Njia hii ya uhimilishaji ni njia bora sana na rahisi kwani inatusaidia kupata mifugo mingi kwa wakati mmoja, inayokua kwa haraka na rafiki kwa mazingira yoyote, husaidia kuepusha magonjwa yasiyo ya lazima, inapunguza ng’ombe wa koo moja kuzaliana (inbreeding), hupunguza hatari kwani wakati mwingine madume huwa makorofi na kusababisha kuumiza wanaowatunza, na kupunguza gharama za uzalishaji,”alifafanua.

Dkt. Mruttu anasema Kambi za uhimilishaji zimechochea hamasa kubwa kwa wananchi kuhimilisha mifugo yao ili kuboresha mbari za mifugo na Wizara inaendelea kufuatilia viwango vya ushikaji mimba kutoka kwenye mikoa husika.

Wakati anatoa wito kwa wafugaji kuhusu uhimilishaji anasema kwa wale wafugaji ambao bado hawajaanza kutumia njia ya uhimilishaji waanze kwani ni njia bora na nzuri na yenye manufaa kwa kila mfugaji mwenye ndoto ya maendeleo na kubadilisha mfumo wa ufugaji na kuwa bora zaidi, Wafugaji wanapaswa kuchangamkia fursa hii ya uhimilishaji kwani ni teknolojia inayoboresha kosaafu za ng’ombe kwa njia rahisi na salama zaidi.

Baadhi ya Wafugaji wameelezea kabla hawaajanza kutumia njia ya uhimilishaji walikuwa hawapati mifugo mingi kama sasa ambavyo wanavyotumia njia hiyo na walidhani ni gharama kutunza mifugo inayopatikana kwa njia ya uhimilishaji tofauti na mifugo ya asili.

Hata hivyo wameelezea mafanikio waliyoyapata kutokana na kutumia njia hii ya uhimilishaji ikiwa ni



**Watafiti kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Utafiti Mafunzo na Ugani Dkt. Ally Hassan Mruttu ( wa tatu kutoka kushoto) wakiangalia mifugo iliyotengwa kwa ajili ya zoezi la uhimilishaji kwenye shamba la KMC LTD wilayani Kyerwa Mkoani Kagera hivi karibuni.**

pamoja na kupata mifugo mingi kwa wakati mmoja, kupata nyama nyingi na maziwa, kusaidia kutunza kosaafu za mifugo yao, kuiongezea thamani na kuvuna mifugo yao ambayo huwapa faida kubwa na kuweza kuendesha maisha yao.

Mwenyekiti wa Wafugaji, Wilayani Kyerwa, Mkoani Kagera, Charles Bwanakunu ameishukuru Wizara kwa kuwasaidia wafugaji wadogo wadogo kuweza kutoka kwenye ufugaji wa kienyeji na kuingia kwenye ufugaji wa kisasa.

"Tunaishukuru serikali kwa kutuelimisha kuhusu uhimilishaji kwani sasa tunafuga kisasa na kwa tija, tumepata ng'ombe bora wanaotoa maziwa mengi na nyama nyingi ukilinganisha na ng'ombe wa asili wanaotoa maziwa chini ya lita moja,"anasema

"Zamani tulikuwa tunatumia gharama kubwa kutunza madume hata kwa miaka mitano lakini njia ya uhimilishaji imetusaidia sana kupunguza gharama hizo na hela tulizokuwa tunazitumia tunafanyia maendeleo mengine,"anaongeza

Anuary Bakhamisi, Mfugaji wa ng'ombe, Wilaya ya Kongwa, Dodoma anasema hana muda mrefu tangu aanze kutumia teknolojia hiyo ya uhimilishaji lakini faida kubwa aliyoanza kuiona ni kupunguza gharama ya kuhudumia ng'ombe madume.

"Faida ninayoweza kusema nimeipata mpaka sasa ni kupunguza gharama za kuhudumia madume, hapo nyuma nilikuwa na madume 20 lakini kupitia elimu hii ya uhimilishaji nimewapunguza mpaka kufikia 5 kwa sababu kupitia njia hii inanifanya nisihitaji madume mengi,"anasema

Bakhamisi anaongeza kuwa anaishukuru wizara kwa kuwapelekea mbegu bora na kupitia kituo cha Uhimilishaji cha NAIC kilichopo Arusha aliweza kununua mbegu bora kwa ajili ya kuhimilisha ngombe wake.

Bwanakunu ambaye ana ng'ombe takribani 300 anaiomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iwe inawapeleka wataalamu wa mifugo mara kwa mara ili kuona wanaendeleaje na wamefikia wapi kutokana na mafunzo waliyoyapata ■



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega (kulia) akishuhudia zoezi la Uhimilishaji kwa Ng'ombe wakati akizindua Kampeni ya Uhimilishaji katika Wilaya ya Kongwa, jijiji Dodoma hivi karibuni.**

# UFUGAJI WA NG'OMBE UNAVYOWEZA KUWA CHANZO MUHIMU CHA NISHATI

Sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta chache ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kukuza pato la Taifa na hata mtu mmoja mmoja. Mpaka kufikia mwaka 2019 sekta ya mifugo imekuwa kwa asilimia 5 na kuchangia asilimia 7.4 katika pato la Taifa.

Kwa kutambua mchango wa sekta ya mifugo Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliamua kuwekeza katika mashamba ya mifugo ili kuyapa uwezo wa kuzalisha mifugo bora itakayosaidia kukuza kipato cha taifa na wananchi wake.

Moja ya shamba ambalo Serikali imewekeza ni shamba la mifugo la Sao Hill lilipo Mkoani Iringa, Wilaya ya Mufindi, Kata ya Ikongosi, Kijiji cha Itulavanu.

## Historia ya Shamba la Sao Hill

Akitoa historia ya Shamba hilo, Kaimu Meneja, Mtama Gerald Galusi anasema kuwa shamba lilianzishwa mwaka 1967 baada ya serikali kulitaifisha kutoka kwa wakulima wa kizungu.

Meneja huyo aliendelea kusema kuwa mwaka 1968 shamba hilo lilianza kufanya kazi rasmi na kutumika kama shamba la kuzalisha mitamba bora 'breeding unit' na kuwauzia wafugaji wadogo wadogo wa Nyanda za Juu Kusini.

Galusi anasema shamba la Sao Hill limekuwa na uzalishaji mzuri kwa sababu shamba hilo linafaidika na hali ya hewa nzuri ya baridi inayowafanya mifugo kustawi vyema na kutoa uzalishaji mzuri tofauti na mashamba mengine ambayo yapo katika ukanda wa joto.

Anasema shamba hilo pia linafaidika na maji ya Mto Ruaha ambao unatiririsha maji kwenye bwawa la Mtera na hivyo mifugo hiyo inapata maji ya kutosha tofauti na mashamba mengine.

## Mafanikio ya Shamba tangu kuanzishwa kwake

Akizungumzia mafanikio ya shamba hilo ambalo lina ng'ombe takriban 1600 (Elfu moja na mia sita), meneja huyo anasema shamba hilo limefanikiwa kuzalisha mitamba mingi na kuisambaza kwa kuwauzia wafugaji wadogo wadogo kwa bei nafuu katika Mikoa ya Iringa na Mbeya na Wilaya zake, huku akisema katika Wilaya ya Rungwe na Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Busokelo Mkoani Mbeya kuna ng'ombe wengi wa maziwa ambao zao lake ni shamba la Sao Hill.



**Mzee Michael Mhosole, mfugaji ambaye pia ni Mkulima wa kijiji cha Igowole, Wilaya ya Mufindi, Mkoa wa Iringa, akionesha jinsi anavyotumia samadi kwa kutengeneza nishati ya gesi ambayo hutumika kwa matumizi ya nyumbani na hivyo kupunguza ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa.**



**Ng'ombe wanaopatikana kwenye shamba la Serikali la Sao Hill Mkoani Iringa.**

Aliongeza kuwa Wilaya hizo zilifaidika na utaratibu waliouanzisha wa Kopa ng'ombe Lipa ng'ombe utaratibu ambao uliwanufaisha wananchi wengi, alisema Meneja huyo.

Aliendelea kusema kuwa shamba hilo limezalisha malisho ikiwa ni pamoja na Mbegu za malisho na kuwauzia wafugaji wadogo wadogo wa Mikoa ya Iringa na Mbeya kwa bei nafuu.

Alisema shamba la Sao Hill linauza ng'ombe wake kwa bei nafuu kwa mfano bei ya Mtamba wenye mimba bei yake ni 1,600,000 (Milioni moja na laki sita) tofauti na mashamba ya watu binafsi yaliyopo katika Wilaya ya Mufindi ambayo bei yake inafika mpaka 3,000,000 (Milioni Tatu) hadi 4,500,000 (Milioni Nne na Laki tano)

Aidha, Meneja huyo ameipongeza Serikali kwa kuwajali na kuwapa wafugaji Mitamba bora kwa bei ambayo kila mtu anaweza kununua.

## Changamoto zinazokabili Shamba hilo

Galusi alisema katika kila mafanikio hapakosi changamoto hivyo alianisha changamoto kadhaa ambazo zinakabili shamba hilo ikiwemo uchache wa vitendea kazi hususan usafiri wa kutembelea maeneo ambayo ina mifugo, alisema kuna baadhi ya maeneo ambayo yapo umbali wa kilomita sio chini ya 10 (kumi) hivyo bila usafiri inakuwa shida kufika katika eneo husika.

Alisema kuwa changamoto nyingine ni kuwa eneo hilo lina mvua nyingi zinazosababisha kupungua kwa madini joto ambayo ni muhimu kwa mifugo jambo ambalo linawalazimu kununua madini hayo kwa bei kubwa.

## Matarajio katika uzalishaji

Kwa upande wa matarajio, Galusi alisema kuwa wanatarajia hadi kufikia Mwezi Juni, 2020 wawe wamesambaza Mitamba aina ya Borani kati ya 120 hadi 130 kwa sababu uhitaji wa ngombe hao bado ni mkubwa.

Alisema Mitamba hiyo Dume aina ya Borani inasaidia kuboresha kosaafu za ng'ombe wa asili kwa wafugaji wadogo wadogo.

## Wito kwa Wadau wa Mifugo

Wito wa Galusi kwa Wadau wa Mifugo ni kwamba wazalishe kwa tija ili wawe na maziwa na nyama za kutosha ili kujenga uwezo wa kusambaza kwenye viwanda ambavyo vinachakata mazao ya mifugo.

Pia, aliwashauri wafugaji kutumia mashamba ya serikali kupata madume bora ili waboreshe kosaafu za mifugo yao pia kuyatumia kama mashamba darasa ya kujifunzia.

Aliendelea kuwashauri wadau wa mifugo kutumia njia ya uhimilishaji kwani inasaidia kuboresha kosaafu za ng'ombe ambao wanakuwa haraka tofauti na ukuaji wa ng'ombe wa Asili.

Robert Semaganga, Afisa Mifugo ambaye pia ni Mratibu wa Sekta ya ng'ombe wa maziwa ameishukuru serikali kwa kuanzisha na kuwekeza katika shamba la Sao Hill kwani limekuwa msaada mkubwa kwa wafugaji huku akitolea mfano shamba la Justine Bimbiga ambaye ana ng'ombe 54 ambao wengi ni zao la shamba hilo na kusema kuwa wanatumia shamba la mfugaji huyo kuonesha matokeo ya shamba la Sao Hill na pia wana vyuo hujifunzia hapo kwa vitendo.

Jobisho Mkonyi, mfugaji wa ng'ombe wa maziwa Wilayani Mufindi alisema kuwa uwepo wa shamba la Sao Hill kumewasaidia kupata Mitamba kwa bei nafuu ambapo Mtamba aliyekuwa anauzwa Milioni Moja na Laki Sita (1,600,000) uongozi wa shamba uliwapunguzia hadi Milioni Moja na Laki Mbili (1, 200,000) na Laki nne walipunguziwa kama ofa kwa wafugaji.

Aliongeza kwa kusema uwepo wa shamba hilo

kunawafanya wapate huduma za wataalamu wa mifugo kirahisi kutoka shambani hapo.

Aidha, aliiomba serikali kuendelea kuwasaidia ili waendelee kupata ng'ombe walio bora zaidi ambao wanatoa maziwa mengi.

## Ushauri wa Serikali kuhusu Malisho

Mkurugenzi wa Idara ya Malisho, Dkt. Asimwe Rwiguza alisema wafugaji wengi bado wanategemea malisho ya asili ambayo kimsingi hayatoshelezi na hayana viini lishe vya kutosha hivyo amewahimiza wafugaji kuandaa mashamba ya malisho na kutumia mbegu bora zinazopatikana kwenye mashamba ya serikali ili kuboresha lishe za mifugo yao.

Aliongeza kuwa Wizara kupitia Idara ya Malisho na Uendelezaji wa Rasilimali za Mifugo imeendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uzalishaji na utunzaji wa malisho.

Faida ya ziada anayoweza kuipata mfugaji wa ng'ombe

Ufugaji wa ng'ombe unaweza kuwa na faida zaidi kama wafugaji wataendelea kupewa elimu ya kutosha kutambua faida nyingine zaidi ya nyama, maziwa na ngozi.

Faida ya ziada anayoweza kuipata mfugaji kutoka kwa ng'ombe aliyefugwa vizuri ni upatikanaji wa nishati ya gesi ambayo kitaalamu inaitwa 'Biogas',nishati hii ya gesi inaweza kupatikana kutokana na kinyesi cha ngombe ambacho wengi wanakiita samadi.

Wafugaji wakielimishwa na kuhamasishwa vizuri kutumia njia hii mbadala ya matumizi ya nishati ya gesi inayotokana na samadi na faida zake huenda itasaidia kupunguza matumizi ya kuni ambayo kwa muda mrefu sasa serikali imekuwa ikiyapiga vita kwani yanatajwa kuwa ni chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira na uoto wa asili nchini.

Katikati ya Mwezi Aprili, 2020 maafisa habari wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi walifanya ziara katika Shamba la Mifugo la Sao Hill ambapo pamoja na mambo mengine walifanya mahojiano maalum na Michael Mhosole, mfugaji na mkulima wa kijiji cha Igowole, Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa ambaye anafanya ufugaji wa ng'ombe wa kisasa kutoka katika shamba la Sao Hill.

Kwenye mahojiano hayo Mhosole alieleza kuwa pamoja na faida ya maziwa anayoipata kutokana na ufugaji wa ng'ombe hao pia anapata nishati ya gesi ambayo anaitumia kwa matumizi ya nyumbani kwake.

Anasema anapata nishati hiyo ya gesi baada ya kujenga mtambo unaotumika kuchakata samadi ya ng'ombe na kuibadilisha kuwa nishati ya gesi tayari kwa matumizi ya kupikia.

Mhosole alisema kuwa nishati ya gesi inayotokana na ng'ombe ikitumika vizuri inasaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Serikali na wataalamu wakiwajengea wananchi uwezo na elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya nishati ya gesi inayotokana na samadi itakuwa ni chanzo kizuri cha ajira kwa vijana.

Aliongeza kwa kusema kuwa baada ya samadi hiyo kutumika kama chanzo cha nishati hutolewa na kupelekwa shambani na kwenda kutumika tena kama mbolea ya kukuzia mazao.

Kwa msingi huo bwana Mhosole aliwahamasisha wafugaji wenzake waone umuhimu wa kutumia nishati hiyo ili wapunguze gharama za matumizi na kutumia kwa usahihi mazao yanayotokana na mifugo ya ng'ombe.

Aidha, alitoa wito kwa wafugaji wenzake na kuwataka wajitahidi kutunza mifugo yao vizuri kwa kuwapatia huduma zinazohitajika ikiwemo kuandaa mashamba ya malisho yatakayowasaidia kuwa na chakula cha kutosha katika kipindi cha kiangazi ambacho kunakuwa na uhaba ■



**Ng'ombe wanaopatikana kwenye shaba la Serikali la Sao Hill Mkoani Iringa.**

# MPINA ASISITIZA MAZINGIRA BORA KWA WAFANYABIASHARA YA MAZIWA NCHINI

Saa kumi usiku wa Juni 25, 2020 Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina alifanya ziara ya kushtukiza katika eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam wanakouza maziwa wajasiriamali wadogo wadogo kwa lengo la kuangalia mazingira ya kazi wanayofanyia biashara wajasiriamali hao ikiwa ni pamoja kutambua changamoto zao.

Katika ziara hiyo Waziri Mpina alisikiliza malalamiko mbalimbali ya wajasirimali hao ikiwemo kuharibiwa maziwa yao kwa kuwekewa rangi na Mafuta ya taa na baadhi ya maofisa wa Bodi ya Maziwa nchini (TDB).

Baada ya kusikiliza malalamiko hayo, Waziri Mpina alihoji hatua ya kuharibu maziwa ya wananchi kwa kuweka rangi na mafuta ya taa iliyofanywa na Bodi ya Maziwa ilizingatia Kanuni gani, jambo ambalo maofisa wa Bodi hiyo walionesha kushindwa kutoa maelezo mazuri ya kifungu kinachowapa mamlaka ya kupima maziwa kwa macho na kuweka mafuta ya taa.

Kufuatia hali hiyo, Waziri Mpina alichukua hatua ya kutengua uteuzi wa aliyekuwa Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Dkt. Sophia Mlote kufuatia kutoridhishwa na utendaji wake wa kazi huku akiagiza maofisa wa Bodi ya Maziwa kusitisha mara moja operesheni ya kuharibu maziwa ya wananchi na badala yake aliwataka kuchukua hatua za haraka za kuwaelimisha wauzaji hao namna bora ya kufanya biashara.

Mmoja wa wafanyabiashara wa maziwa, Ester Elius alimueleza Waziri Mpina kuwa zoezi hilo lililofanywa la kuwawekea mafuta ya taa na rangi kwenye maziwa limewasababishia hasara kubwa na kuomba serikali kuwasaidia mikopo ili waweze kukidhi matakwa ya kisheria yanayotakiwa na bodi hiyo ikiwemo kutumia vyombo vinavyoshauriwa kitaalamu.

Baada ya ziara hiyo, Waziri Mpina alimuagiza Mratibu wa Dawati la Sekta Binafsi la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Michael kukutana na wajasirimali hao ili kutambua mahitaji yao ya kifedha na kuwaunganisha na Taasisi za kifedha kwa ajili ya kupatiwa mikopo ili waweze kufanya biashara zao kwa tija ■



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Luhaga Mpina (kushoto) akisikiliza kero za wafanyabiashara wadogowadogo katika eneo maalum la kuuzia maziwa lililotengwa kwa ajili ya wafanyabiashara hao lililopo Ubungo jijini Dar es Salaam hivi karibuni.**

# FAHAMU FAIDA ZA UHAWILISHAJI KATIKA SEKTA YA MIFUGO

## Uhawilishaji ni nini?

UHAWILISHAJI ni kitendo cha kupeleka au kusambaza teknolojia ya mifugo kwa wadau au wafugaji ili ianze kutumika. Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Taasisi ya utafiti wa Mifugo (TALIRI) inaratibu zoezi la Uhawilishaji wa teknolojia za mifugo ili kuongeza ufugaji wenye tija nchini.

Kihistoria uhawilishaji wa teknolojia za mifugo ulianza enzi za ukoloni katika kituo cha Mifugo Mpwapwa. Kwa sasa uhawilishaji unahusisha wigo mpana ikiwemo Ng'ombe aina ya Mpwapwa breed, na Freisian, pia Mbuzi aina ya Malya (blended goats) na kuku aina ya sasso na kuloirer.

Lengo la kufanya uhawilishaji ni kuongeza upana wa matumizi ya teknolojia ya mifugo kwa wadau wengi kutoka kwenye chanzo kilichogundua teknolojia hiyo. Vilevile kuongeza matumizi ya teknolojia kibiashara na kuboresha ufanisi wa mifumo ya uzalishaji.

Wizara imeweka utaratibu wa ununuzi wa vifaa vya viinitete (Multiple ovulation and Embryo Transfer (MOET), unaofadhiliwa na serikali ya Tanzania kupitia Tume ya Taifa ya sayansi na Technolojia (COSTECH)




**Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Dkt. Eliggy Shirima akionesha teknolojia ya uhawilishaji inayotumika kuboresha na kuongeza idadi ya mifugo nchini.**

ambavyo vinasaidia kumwezesha ng'ombe jike kuzalisha viinitete 8 mpaka 450 kwa mwaka. Kutokana na ununuzi wa vifaa hivyo, vimesaidia kuzalisha, kuhifadhi na kufungasha viinitete kwa ajili ya uhimilishaji na uhawilishaji.

Katika hatua za uhawilishaji, TALIRI hufanya utafiti wa vituo ili kutathimini ubora wa teknolojia (on station Research), kufanya tathimini kwa wafugaji wachache (contact farmer-on farm Research), na kuzalisha kwa wingi teknolojia zinazofaa na kusambaza kwa umma.

Mkurugenzi wa TALIRI, Dkt. Eligy Shirima anasema uhawilishaji huongeza ufanisi katika ufugaji, kwa kuongeza kipato kwa wafugaji na taifa kwa ujumla kwa sababu uzalishaji wa mifugo bora unafanyika katika kanda tofauti na kwa wingi.

"Kwa kila mwaka TALIRI huwafikia wafugaji zaidi ya elfu moja (1000) na mwitikio wa wafugaji ni mkubwa sana ukilinganisha na miaka ya nyuma na huongezeka mwaka hadi mwaka na kufanya uhumilishaji kusambaa kwa upana zaidi, Kwa ujumla wafugaji wameitikia vizuri ushauri na elimu wanayopewa inayolenga kuongeza tija katika uzalishaji,"anasema Shirima

"Wadau wengi wanafuatilia ili kupata mbegu bora za kuku, Ngombe, Mbuzi na mifugo mingine. Wizara kupitia TALIRI ilitoa mafunzo kwa maafisa ugani 19 ambao walihimilisha Ngombe 810 na kupima ili kuthibitisha mimba za Ngombe 1,034,"aliongeza Shirima.

Akizungumzia changamoto za uhawilishaji wa teknolojia, Dkt. Shirima amesema bado baadhi ya wafugaji hawana mabanda bora, hawatunzi vizuri kumbukumbu mbalimbali za mifugo, uwezo mdogo wa wafugaji unaosababisha baadhi yao kutowapa mifugo chakula cha kutosha na tatizo la umakini na utekelezaji wa ushauri au maelekezo juu ya ufugaji wenye tija endelevu yanayotolewa na wataalam wanapowatembelea.

Aidha, katika uhawilishaji wa teknolojia wadau na wafugaji wanakumbana na changamoto ya kutopata mbegu/vifaa kwa idadi wanayotaka na kwa wakati.

Kutokana na changamoto hiyo, Dkt. Shirima anasema wizara kupitia taasisi zake inaendelea kuongeza uwezo wa uzalishaji wa teknolojia mbalimbali na kuzisambaza kwa wadau ili kukidhi mahitaji yao.

Dkt. Shirima anasema uhaba wa rasilimali fedha za kufanya tafiti ili kuzalisha teknolojia na kuzisambaza unafanya wafugaji kukosa mahitaji kwa wakati na kwa kiwango wanachohitaji ■



**Baadhi ya ndama waliozaliwa kwa kutumia teknolojia ya uhimilishaji, walioko kwenye shamba la mfugaji Dotto Lushu wa Kisarawe mkoani Pwani.**

# BODI YATAKIWA KUBUNI NJIA ZA KUBORESHA HUDUMA ZA LITA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel ameitaka Bodi Mpya ya Ushauri ya Wakala ya Vyuo vya Mifugo(LITA) kuwa bunifu ili kuboresha huduma na kuleta tofauti katika shughuli zao na kufikia malengo yake.

Prof. Gabriel aliyasema hayo alipokuwa akifungua kikao cha kwanza cha Bodi mpya ya ushauri ya LITA kilichofanyika jijini Dar es Salaam Julai 25, 2020.

Akizungumza katika kikao hicho, Prof. Gabriel aliwahimiza wajumbe wa bodi hiyo kutumia vyema taaluma zao na kuwa wabunifu katika kuhakikisha LITA inaboresha huduma zake na kuleta mabadiliko chanya ya kiutendaji ya Wakala hiyo.

"Nawaomba bodi mfanye kazi yenu vizuri na mfanye maboresho kadri itakavyowezekana, shirikianeni kwa ukaribu na wadau wengine ili kusaidia kuboresha shughuli zenu," alisema Prof. Gabriel

Sambamba na hilo, Prof. Elisante ameitaka bodi hiyo kuhakikisha inasimamia vyema rasilimali fedha za taasisi hiyo huku akiwaeleza kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Luhaga Mpina wakati wote amekuwa



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala ya Vyuo vya Mifugo (LITA) muda mfupi baada ya kufungua kikao chao cha kwanza tangu wasimikwe Julai 6, 2020, kilichofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia (waliokaa) ni Mwenyekiti wa Bodi ya LITA, Prof. Malongo Mlozi na Kushoto ni Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa LITA, Dkt. Pius Mwambene. Waliosimama kutoka kulia ni wajumbe wa Bodi hiyo, Wa kwanza ni Dkt. Angello Mwilawa, wa pili ni Bi. Josephine Matiro, katikati ni Prof. Zacharia Masanyiwa. Kutoka kushoto (wa kwanza) ni Bw. Mark Tsoso na anayefuata ni Bi. Faraja Makafu.

mkali na watu ambao wamekuwa wanatumia vibaya rasilimali za umma.

Aliendelea kueleza kuwa ili LITA waweze kufanikiwa katika shughuli zao ni vyema wakaweka mikakati ya kuboresha eneo la masoko na habari ambalo litasaidia kutangaza na kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari kutumia huduma zinazotolewa na LITA ili kuongeza mapato yake.

"Hii ni taasisi ya biashara hivyo ni muhimu kuitangaza vya kutosha ili watu waijue LITA ni nini, ipo wapi na inafanya nini, kwa kufanya hivyo kutaivuta jamii kutumia huduma zenu," alifafanua

"Serikali inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli imefanya kazi kubwa mpaka sasa tumeingia katika uchumi wa kati, hivyo LITA ni lazima muhakikishe mnaenda sambamba na kasi hii ya uchumi wa kati kwa kuboresha huduma zenu ikiwemo kubuni vyanzo vingine vya mapato," aliongeza

Akiongea mapema katika kikao hicho, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Vyuo vya Mifugo(LITA), Dkt. Pius Mwambene alisema kuwa mpaka sasa taasisi hiyo imepata mafanikio kadhaa ikiwemo kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi kutoka 798 mwaka 2012/13 hadi kufikia 3642 mwaka 2019/2020 huku akisema kuwa wameshaongeza Kampasi nyingine mbili ambazo ni Mabuki, Mwanza na Kikulula, Kagera.

"Kuanzia Mwaka jana tumeanza kutoa gawio katika mfuko mkuu wa Serikali ambapo tulianza kutoa kiasi cha shilingi milioni 50 mwaka jana na mwaka huu tumetoa milioni 100,"alifafanua Dkt. Mwambene

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya LITA, Prof. Malongo Mlozi alisema kuwa kufuatia kauli hiyo ya Katibu Mkuu watahakikisha kuwa wataweka utaratibu kwa kushirikiana na Menejimenti kuangalia mapato na matumizi ya fedha kila miezi mitatu huku akieleza kuwa kwa nafasi yao wataendelea kutoa ushauri juu ya matumizi bora ya rasilimali umma.

Kuhusu suala la ubunifu alisema kuwa wataweka mipango mizuri kuhakikisha taasisi hiyo kupitia Kampasi zake inajiendesha kibiashara ili kujiongezea kipato ■



**Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel akiongea na Wajumbe wa Bodi Mpya ya Ushauri ya Wakala ya Vyuo vya Mifugo (LITA) wakati akifungua kikao cha kwanza cha bodi hiyo kilichofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.**

# MAAFISA UVUVI WATAKIWA KUSIMAMIA SHERIA ILI KUONGEZA PATO LA TAIFA

Sekta ya Uvuvi ni moja kati ya sekta muhimu za kiuchumi hapa nchini ambayo inahusisha uvuvi kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe maji ambapo katika mwaka 2019, sekta hiyo ilichangia asilimia 1.71 ya pato la Taifa na imekua kwa asilimia 1.5.

Inakadiriwa kuwa zaidi ya Watanzania milioni 4.5 wanategemea shughuli zinazohusiana na uvuvi ambazo huwasaidia wananchi kuwa na uhakika wa lishe, kuongeza kipato ikiwemo fedha za kigeni na kupunguza umaskini.

Katika kuhakikisha sekta hiyo inakuwa endelevu serikali imekuwa ikitunga sheria na kanuni mbalimbali ili kusimamia shughuli za uvuvi kwa wadau wa sekta hiyo ambapo baadhi ya sheria na kanuni hizo zimekuwa zikifanyiwa marekebisho kuendana na hali halisi ya mabadiliko ya mahitaji kwa wakati husika.

Mwezi Februari, 2020, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega alipofanya ziara ya kikazi ya siku mbili Mkoani Tanga na kukutana na wadau wa sekta ya uvuvi katika Wilaya za Pangani na Halmashauri ya jiji la Tanga aliwataka wavuvi kuheshimu sheria katika maeneo husika ambayo wanafanyia shughuli za uvuvi ili kuondoa migogoro kati yao na maafisa wanaosimamia shughuli hizo.

Kwa nyakati tofauti akiwa katika wilaya hizo, Naibu Waziri Ulega, alipokea maoni na maswali kutoka kwa baadhi ya wadau wa sekta hiyo ambapo baadhi ya mambo ni juu ya ukomo wa maeneo ya kuvua samaki katika Bahari ya Hindi kwa kutumia sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akijibu hoja hiyo Naibu Waziri Ulega aliwaambia wadau wa uvuvi kuwa sheria za Wizara ya Mifugo na Uvuvi hazivuki kufanya kazi katika serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwamba sheria za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi za serikali ya Mapinduzi Zanzibar pia hazivuki kufanya kazi katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi mhe. Abdallah Hamis Ulega akiwa na baadhi ya wadau wa sekta ya uvuvi mkoani Tanga mara baada ya kuzungumza nao kuhusu maendeleo ya sekta hiyo hivi karibuni.**

Aidha, Waziri Ulega aliwaambia wadau wa uvuvi kuwa leseni ya uvuvi inamruhusu mvuvi kuvua samaki katika maeneo yeyote hapa nchini ikiwemo Bahari ya Hindi, maziwa na mito ili mradi azingatie sheria ndogo ndogo za maeneo husika.

Aliwataka pia maafisa uvuvi nchini kusimamia vyema sheria, kanuni na taratibu katika sekta ya uvuvi nchini bila kuwaonea wadau wa sekta hiyo ili iongeze tija zaidi kwa wadau hao.

“Maafisa uvuvi ninawaagiza hakikisheni mnasimamia sheria, na pia mtende haki, msimuonee mtu yeyote na watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa tutawachukulia hatua za kisheria.” alisema.

Baadhi ya wadau wa sekta ya uvuvi walimuomba pia Naibu Waziri kuwatatulia changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo zikiwemo za wingi wa tozo, mikopo na elimu ya vifaa sahihi vinavyotakiwa katika shughuli za uvuvi ili kujiepusha na vitendo vya uvuvi haramu bila kukusudia.

Kuhusu matukio ya uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi wadau wa sekta ya uvuvi Mkoani Tanga waliamuarifu Waziri Ulega kuwa wamekuwa wakishirikiana na maafisa mbalimbali wa serikali kutokomeza vitendo hivyo na kwamba wameweza kutokomeza matukio hayo katika maeneo yao.

Akitoa tathmini kwa mwaka 2019, Waziri Ulega aliwaambia kuwa serikali kwa kushirikiana na wavuvi imeweza kutokomeza matukio ya uvuvi haramu ukiwemo wa kutumia mabomu katika Bahari ya Hindi na kwamba serikali itaendelea kusimamia na kudhibiti matukio hayo na kwamba itasimamia sheria kwa yeyote atakayekamatwa akihusika na matukio hayo.

Aidha, Wadau hao kwa ujumla wamepongeza namna Wizara ya Mifugo na Uvuvi inavyosimamia maslahi ya wavuvi yakiwemo ya kuhakikisha wadau wa sekta hiyo wanapatiwa mikopo kupitia taasisi mbalimbali za kifedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ■



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega akisikiliza kero ya ukosefu wa soko la dagaa kutoka kwa mmoja wa wavuvi aliokutana nao mkoani Tanga wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya sekta ya Uvuvi, hivi karibuni.**

# SERIKALI YAPONGEZWA KWA ULINZI WA RASILIMALI ZIWA VICTORIA

- ***Waziri Mpina achoma nyavu haramu zaidi ya 100,000***
- ***Serikali yataifisha boti 11 za Uvuvi haramu***
- ***Serikali kutoa milioni 10 kila mwezi kwa mkoa wa Mara ili kuimarisha ulinzi na doria katika ziwa Victoria***

“Serikali ya awamu ya tano ilipoanza doria ya kusaka zana za uvuvi haramu, wananchi hatukuelewa tukaona serikali yetu inatuonea, lakini baada ya muda sasa tumeona mafanikio yake kwani samaki wameongezeka kwa idadi na kwa ukubwa hata viwanda kwa sasa vinapata samaki wa kutosha na ajira zimeongezeka” hayo yamesemwa na Bwana Amosi Matiku mkazi wa Tarime Mkoani Mara.

Naye Fausta Abeli mjasiriamali wa samaki jijini Mwanza anasema kwa wingi wa samaki hata bei imeshuka kwa samaki, akitolea mfano wa samaki aina ya sato Bi.Fausta anasema kwa sato waliokuwa wanauzwa sh.7000/- kwa sasa unaweza kuwapata hata kwa sh.5,500/-, kwa hiyo sisi wajasiriamali na walaji wa kitoweo hicho tunashukuru na faida ya operesheni sangara tumeiona.

Suala la Ulinzi huu wa rasilimali zilizopo kwenye maji asili lilitiliwa mkazo kwenye Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambapo alielekeza wizara ya Mifugo na Uvuvi kuweka mikakati ya utekelezaji wa azma hiyo, ndipo wizara ilipoanza operesheni Sangara katika Ziwa Victoria.

Katika kuendelea kuhakikisha Sekta ya Uvuvi inatoa mchango mkubwa katika kuliingizia mapato Taifa ikiwemo fedha za kigeni, Juni 29, 2020 Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Luhaga Mpina alichoma nyavu



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Luhaga Mpina (wa nne kutoka kulia) akisimamia na kushuhudia zoezi la uchomaji nyavu haramu alililoendesha katika mikoa ya Kanda ya ziwa (Mwanza na Geita) hivi karibuni.**

laki moja na elfu kumi (110,000) zilizokuwa zikitumika kwenye uvuvi haramu ndani ya ziwa Victoria.

Wakati huohuo, Waziri Mpina amewaonya wanasiasa watakaotumia kampeni kuwahadaa wananchi na uvuvi haramu kuwa watakamatwa wakiwa majukwaani.

"Natoa onyo kwa wanasiasa kuacha kulihusisha jambo la uvuvi haramu na mambo ya kampeni, kama wanataka umaarufu watafute kwa njia nyingine na sio kwa kuwahadaa wananchi na mambo ya uvuvi, hatuna utani, hizi ni rasilimali za Watanzania," alisema

"Yeyote anayedhani serikali haitachoma nyavu na haitakamata wavuvi haramu kwa ajili ya kupata kura kwenye uchaguzi mkuu ujao anajidanganya,"alionya Mpina.

Aidha, katika opresheni hiyo, Serikali imetaifisha boti 11 zilizokuwa zikifanya uvuvi kinyume cha taratibu ndani ya Ziwa Victoria Mkoani Mara, huku boti saba zikiwa ni za nchi jirani.

Serikali pia imefanikiwa kuteketeza nyavu zaidi ya laki moja na elfu kumi (110,000) ambazo pia zilikamatwa katika ziwa hilo.

"Ili kuhakikisha kuwa, mapambano dhidi ya uvuvi haramu yanakuwa endelevu, serikali itaanza kutoa Tsh. 10 milioni kila mwezi kuanzia mwezi Julai, mwaka huu kwa mkoa wa Mara ili kuimarisha ulinzi na doria katika ziwa Victoria," alifafanua.

Naye, Afisa Mfawidhi wa Usimamizi na Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi mkoa wa Mara, Samson Mboje amesema kuwa wamefanikiwa kukamata watu 24 wakijihusisha na uvuvi haramu, ambapo 18 ni kutoka nchi ya Kenya, watatu kutoka Uganda na watatu Tanzania na watuhumiwa wote walifikishwa mahakamani ■



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, mhe. Luhaga Mpina akiongoza zoezi la uchomaji wa nyavu zinazotumika kwenye uvuvi haramu kwenye mikoa ya kanda ya ziwa (Mwanza na Geita) hivi karibuni. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi (WMUV) Bw. Emmanuel Bulayi.**

# WAVUVI WAISHUKURU SERIKALI KWA KUWAPATIA MKOPO

- ***Azma ya serikali ni kuona mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la taifa unaongezeka kutoka Asilimia 1.7 hadi 2 ya sasa na kufikia Asilimia 5 na kuendelea***
- ***Vyama vya Ushirika vya Wavuvi vyaishukuru Serikali kwa kuwaamini***

Katika kutekeleza azma yake ya kuwainua kiuchumi Wavuvi, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais, Dkt. John Magufuli imeweka mikakati mizuri ya kuhakikisha Wavuvi wanaanza kuaminika na kukopeshwa kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Katika kutimiza hilo, hivi karibuni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akiwa katika Wilaya za Ukerewe na Sengerema Mkoani Mwanza alikabidhi jumla ya mkopo wa Shilingi Milioni 300 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa Chama cha Ushirika wa Wavuvi Bukasiga kilichopo Wilayani Ukerewe na Chama cha Ushirika cha Zilagula kilichopo Wilayani Sengerema.

Akizungumza katika Kijiji cha Kanyala kilichopo Halmashauri ya Buchosa iliyopo Wilaya ya Sengerema Mkoani Mwanza, wakati wa kukabidhi mkopo wa Shilingi Milioni 100.7 uliotolewa na TADB kwa Chama cha Ushirika cha Zilagula ambacho pia kimepata mkopo wa Shilingi Milioni Tano kutoka katika mfuko




**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega akionesha mfano wa hundi wakati akikabidhi mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa Chama cha Ushirika cha Zilagula kilichopo Wilayani Sengerema, Mkoani Mwanza hivi karibuni.**

wa mapato ya ndani ya halmashauri hiyo, Naibu Waziri Ulega alisema licha ya vyama vingine vya Kasalazi na Soswa ambavyo kila kimoja kimepata pia mkopo wa halmashauri wa Shilingi Milioni Tano, ili wafugaji na wavuvi waweze kunufaika na mikopo kupitia ushirika wao, wizara itakuwa msimamizi kwa vyama vitakavyokidhi sifa za kupata mikopo kutoka TADB.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaenda kuwa msimamizi namba moja wa vyama vya ushirika tena kwa barua hivyo niwatakeni uongozi wa mkoa, halmashauri na ushirika wekeni taarifa zenu vizuri. Tunataka viwanda vidogo vidogo vya wafugaji na wavuvi vikiwemo vya kukausha dagaa, minofu ya samaki na kutengeneza kayabo nzuri ili mpeleke bidhaa hizo kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi." Alisema Ulega

Pia, amevitaka vyama hivyo vitatu vilivyopata mikopo kuitunza kwa kuifanyia kazi na hatimaye kuirejesha kwa kuwa fedha zilizotolewa na benki hiyo zinamilikiwa na Watanzania kwa asilimia mia moja, hivyo wakirejesha watanzania wengine pia watanuifaika na mikopo hiyo.

Wakati akikabidhi hati ya kuandikishwa kwa vyama vya Sangara-Nyakaliro na Gembare vilivyopo Halmashauri ya Buchosa Ulega aliwasihi wavuvi kuendelea kujiunga katika vyama vya ushirika huku wakati akiwataka watendaji wa serikali kutoa elimu kwa vyama vya ushirika namna ya kuitumia vyema mikopo wanayopata ili waweze kuirejesha kwa wakati na kuwaongoza ili waweze kupata mikopo mikubwa zaidi.

"Watendaji wakati mwingine vyama vya ushirika havikosei kufikia hatua mbaya ya kukosa mikopo ni muhimu elimu itolewe na watendaji kwa wafugaji na wavuvi, msiwaache hawa watu wa ushirika waliopatiwa mikopo waelimisheni na kuwaongoza hatua kwa hatua ili waweze kulipa marejesho ya mikopo waliyopatiwa", Alifafanua

Vilevile, Naibu Waziri Ulega amewataka viongozi wa vyama vya ushirika kujiepusha na ubadhirifu wa fedha za mikopo hiyo kutoka TADB, huku akitoa rai kwa wavuvi kuwa na uchumi endelevu na hatimaye kuwa walinzi wa rasilimali za uvuvi kupitia vyama vyao vya ushirika.

"Azma ya serikali ni kuona Tanzania inaongoza kwa kusafirisha minofu ya samaki kwenda nje ya nchi na mchango wa samaki katika pato la taifa unaongezeka kutoka Asilimia 1.7 hadi 2 ya sasa na kufikia Asilimia 5 na kuendelea",

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) Bw. Japhet Justine ameishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuweka mikakati mizuri na benki hiyo iliyowezesha na kuhakikisha wafugaji na wavuvi wanakuwa na sifa za kupatiwa mikopo ili kujiendeleza katika sekta hizo.

"Tuliomba kwanza vyama hivi vikae katika ushirika kwa sababu tuliamini ule umoja wao utatupatia njia kuhakikisha mikopo inalipwa kwa kuwaweka katika mfumo ulio rahisi, wizara pia iliweka mazingira ya kubadilisha mitumbwi kuwa na namba na kufahamika ili benki iweze kuwa na taarifa sahihi ya mitumbwi ya wahusika wanaopatiwa mikopo pamoja na kuweka mazingira ya wavuvi kuwa na mifumo rasmi ya kuweka na kutoa pesa ili benki iweze kujua historia na kutoa mikopo kulingana na historia ya waombaji", alibainisha Justine.

Aliongeza kuwa nia ya TADB ni kuona wafugaji na wavuvi wengine wengi wananufaika na mikopo hiyo, hivyo aliwataka wavuvi na wafugaji kufanya biashara zao kwa kuweka kumbukumbu zao vizuri ili wanufaika waweze kufikia hatua ya kuwa na viwanda vidogo vidogo.

Aidha, amesisitiza kwa vyama vya ushirika vilivyopata mkopo kutoka TADB kuhakikisha vinalipa mikopo hiyo kwa wakati ili watanzania wengine wenye uhitaji wa kupata mikopo hiyo waweze kupata na kukuza biashara zao.

Kuhusu Dawati La Sekta Binafsi lililo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambalo limekuwa likifanya kazi kubwa katika kuhakikisha wafugaji na wavuvi wanaunganishwa na taasisi mbalimbali za kifedha, Mratibu wa Dawati hilo, Steven Michael amesema kazi yao kubwa ni kuhakikisha matokeo chanya yanaonekana likiwemo tukio la Chama cha Ushirika cha Zilagula kupatiwa mkopo wa Shilingi Milioni 100.7 kutoka TADB.

Michael amesema wamefanya kazi kubwa kuhakikisha vyama vya ushirika vinaunganishwa na taasisi za kifedha pamoja na halmashauri mbalimbali nchini na kuvifuatilia mara kwa mara kwa kuwa kazi yao kubwa ni kuwaunganisha wadau wa mifugo na uvuvi na taasisi hizo kifedha pamoja na serikali.

Akizungumza baada ya kupatiwa mkopo huo, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Zilagula, Joram Yuda alisema wanaishukuru serikali kwa kuwa wavuvi wameanza kuaminika na taasisi za kifedha kwa kuwapatia mikopo ili kujiendeleza katika sekta hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Gembare, Hassan Muhenga ameishukuru pia Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na TADB kwa kuhakikisha wanasimamia maono ya Rais Dkt. John Magufuli ya wavuvi kupatiwa mikopo.

Akiwa katika Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya mkopo wa

Shilingi Milioni 200 kwa Chama cha Ushirika cha Wavuvi Bukasiga kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha barafu, Naibu Waziri Ulega alifafanua kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli ameweka mazingira ya kufanya wavuvi waweze kuaminika na taasisi za kifedha na kupewa mikopo ili kujiimarisha katika shughuli zao.

"Hii benki tangu ianze ina miaka mitano sasa na katika miaka mitano ya Dkt. John Magufuli imewakopesha watanzania katika nyanja za kilimo, mifugo na uvuvi zaidi ya Shilingi Bilioni 170 na tangu uhai wa taifa hili wavuvi wameanza kuaminika na kukopeshwa pesa", alisisitiza.

Waziri Ulega aliongeza kuwa wavuvi walikuwa wanaonekana ni watu wa kuhamahama lakini kwa uthubutu, uzalendo na utayari wavuvi wanaanza kuaminika na kuhamasishwa kujiunga katika vikundi vya ushirika na kupatiwa mikopo ya masharti nafuu ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020, ibara ya 27 na msimamo wa Rais Dkt. John Magufuli.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo Tanzania (TADB), Japhet Justine akizungumza katika hafla hiyo fupi ya kukabidhi mkopo wa Shilingi Milioni 200 kwa Chama cha Ushirika wa Wavuvi Bukasiga kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha barafu, amesema wameweza kutekeleza upatikanaji wa mkopo huo baada ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuweka mikakati ya kuhakikisha inatekeleza uvuvi uwe wa kisasa utakaoonesha fursa zaidi.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wanachama wa kikundi cha Bukasiga, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Jumbula Lugola amesema wanashukuru kwa mkopo huo kwa kuwa shughuli zao za uvuvi zitabadilika na kufanyika kisasa zaidi kwa kuwa CCM imeweka mkakati mzuri ili kuhakikisha wavuvi wananufaika kupitia mikopo.

Ameongeza kuwa kwa juhudi za Rais Magufuli hatimaye wameweza kupatiwa mkopo na TADB wa Shilingi Milioni 200 na kumuahidi Rais Magufuli kuwa mkopo waliopatiwa watahakikisha wanautumia vyema ili uwanufauishe pia watanzania wengine ■



**Lengo la mikopo ni kuwainua wavuvi kiuchumi kwa kupata zana bora za kufanikisha shughuli zao za kila siku.**

# KIWANDA CHA KUCHAKATA SAMAKI RUKWA CHAJENGWA

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais, Dkt. John Magufuli toka iingie madarakani mwaka 2015 imeweka msukumo mkubwa katika ujenzi wa viwanda ili kusaidia nchi kufikia uchumi wa kati.

Msukumo huo umeendelea kupokewa vizuri na wawekezaji wa ndani na wa nje zikiwemo sekta binafsi na taasisi za serikali. Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta ambazo zimeisimamia vizuri sana kauli mbiu hii ya uchumi wa viwanda.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah mpaka sasa vimeshaanzishwa viwanda vya kuchakata samaki takribani 18 ambapo viwanda 10 vipo Kanda ya ziwa na viwanda 8 vipo katika Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi.

Katika kuhakikisha viwanda vinaendelea kujengwa nchini, Rais, Dkt. John Magufuli alipofanya ziara katika Mikoa ya Katavi na Rukwa mwaka jana aliitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha kuwa katika ukanda huo wa ziwa Tanganyika kunaanzishwa kiwanda cha kuchakata samaki ili kuwasaidia wavuvi wa maeneo hayo kupata soko la uhakika la samaki.

Kufuatia agizo hilo, Kampuni ya Alpha Tanganyika Flavour kupitia ushirikiano mkubwa kutoka kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wameweza kufanya uwekezaji katika sekta hiyo ya uvuvi kwa kuanzisha kiwanda cha kuchakata samaki ambacho kwa sasa kinamalizia ukarabati wake kabla ya kuanza kazi mwishoni mwa mwezi wa tisa, mwaka huu.

Katika kuhakikisha uwekezaji huo unafanyika kwa kukidhi vigezo vya kitaalam, Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi(Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah alifanya ziara ya kukagua ukarabati wa kiwanda hicho cha kuchakata samaki cha Alpha Tanganyika Flavour kilichopo Wilayani Sumbawanga, Mkoani Rukwa Agosti 13, 2020.



**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (wa tano kutoka kushoto, aliyevaa koti jeusi), akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji, Alpha Tanganyika Flavour, Alpha Nondo (aliyevaa T-shirt ya njano) alipotembelea kiwanda cha Alpha kilichopo Mkoani Rukwa kukagua ukarabati wake unaoendelea hivi karibuni. Wengine pichani ni Wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Maafisa wa Kampuni ya Alpha Tanganyika Flavour.**

Akiwa katika kiwanda hicho, Dkt. Tamatamah alisema kuwa ujenzi na ukarabati wa kiwanda hicho ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Magufuli aliyoyatoa katika ziara yake mwaka jana kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha kuwa katika Mkoa huo kunaanzishwa kiwanda cha kuchakata samaki ili kuwaondolea kadhia ya masoko wanayoipata wavuvi wa maeneo hayo na mikoa ya jirani.

"Leo nimekuja na wataalamu wangu kukagua ukarabati unaoendelea katika kiwanda hiki cha Alpha ambapo ukikamilika na kiwanda hiki kuanza kazi kitatoa ajira zaidi ya mia moja (100) kwa wananchi na vile vile kitachangia kuongeza mapato ya Serikali,"alisema Dkt. Tamatamah.

Dkt. Tamatamah aliendelea kueleza kuwa kiwanda hicho kikikamilika kitakuwa ni kiwanda cha 19 na kitakuwa kiwanda cha kwanza kikubwa katika ukanda wa ziwa Tanganyika, na kitakuwa na uwezo wa kuchakata Tani 20 za samaki ambazo bidhaa zake zitauzwa ndani ya Tanzania na nje hususan katika soko la Marekani na hivyo kitasaidia nchi kupata fedha za kigeni.

Dkt. Tamatamah aliongeza kuwa kiwanda hicho kitasaidia kupunguza utoroshaji wa samaki nje ya nchi ambao kwa kiasi kikubwa unaendelea kuikosesha serikali mapato.

Aidha, Dkt. Tamatamah alitumia fursa hiyo kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo ya Alpha Tanganyika Flavour, Alpha Nondo kwa kuamua kufanya uwekezaji huo mkubwa ambao unatekeleza kwa vitendo agizo la Rais Magufuli huku akimuahidi kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi itaendelea kumpatia ushirikiano utakaohitajika ili kumuwezesha kufikia azma yake ya kuwekeza kiwanda hicho mkoani humo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji, Alpha Tanganyika Flavour, Alpha Nondo aliishukuru Serikali kwa ushirikiano mkubwa anaopatiwa huku akisema kiwanda hicho kitakuwa ni jibu kwa Rais Magufuli na Wavuvi waliokuwa wanahangaika na soko la kupeleka samaki wao.

"Kiwanda cha Alpha kinakuja kumkomboa mvuvi aliyekuwa hana uhakika na soko la samaki wake, hivyo nawaomba wavuvi na wananchi wote kutupa ushirikiano ili kiwanda hiki tunachoenda kukianzisha kiweze kuwahudumia vizuri,"alisema Nondo.

Naye, Katibu Tawala Msaidizi, Mkoani Rukwa, Ocrani Chengula alisema kuwa kwa muda mrefu Mkoa huo ulikuwa unahangaika kupata kiwanda cha kuchakata samaki ili kiweze kuwasaidia wavuvi kupata masoko ya uhakika na kuachana na kufanya biashara ya kutorosha samaki kiholela katika nchi za jirani.

"Tunaamini kuanzishwa kwa Kiwanda hiki, kwanza kitatoa ajira kwa watu wetu hapa, lakini vile vile kitatuongezea mapato katika Halmashauri yetu na pia Wavuvi wetu wataachana na uuzaji holela wa samaki wao kwa sababu soko la uhakika litakuwa limepatikana kupitia Kiwanda hiki,"alifafanua Chengula ■




**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (katikati) akiongea na Waandishi wa habari (hawapo pichani) alipotembelea na kukagua ukarabati wa kiwanda cha Alpha Tanganyika Flavour kilichopo Mkoani Rukwa hivi karibuni. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji, Alpha Tanganyika Flavour Ltd, Alpha Nondo. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi (WMUV), Stephen Lukanga.**

# WIZARA KUJENGA VITUO VYA KUZALISHIA SAMAKI

Katika hatua za kuimarisha Sekta ya Uvuvi nchini, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepanga kukarabati na kupanua vituo sita (6) vya kukuzia na kuendeleza Viumbe Maji ili viweze kuzalisha vifaranga milioni nane (8).

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji, Dkt. Nazael Amos Madalla anasema lengo la kujenga vituo hivyo ni kuhamasisha na kuendeleza tasnia ya ukuzaji viumbe kwa kutoa elimu ya mbinu bora za ukuzaji viumbe maji na kuzalisha vifaranga vya samaki ili kuboresha lishe, kipato, ajira na mchango wa sekta ya Uvuvi kwenye pato la Taifa.

Maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa vituo hivyo ni pamoja na Mwamapuli-Tabora, Ruhila-Ruvuma, Kingolwira-Morogoro, Nyengedi-Lindi, Machui-Tanga na Rubambagwe-Geita.

Dkt. Madalla anasema katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Vitotoleshi vya Serikali vinatarajiwa kuzalisha vifaranga milioni 8 na watahamasisha Sekta Binafsi ili kuzalisha vifaranga milioni 22 na hivyo kufanya vifaranga vyote kufikia milioni 30 kwa mwaka.

Anasema kupitia vituo hivyo Idara itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika kuzalisha vifaranga vya samaki na kutakuwa na mashamba darasa kwa ajili ya kutoa elimu ya ufugaji bora wa samaki kwa jamii.



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Abdallah Ulega (kushoto) akipata maelezo kuhusu ufugaji wa jongoo bahari alipotembelea kituo cha ututoleshaji vifaranga vya samaki, jongoo bahari na kaa mjini Unguja, Zanzibar Juni 2, 2020. Katikati ni Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili na Uvuvi wa SMZ, Dkt. Makame Ali Ussi.**

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kuanzia mwaka 2015 mpaka sasa Wizara inajivunia kufikia mafanikio mbalimbali katika sekta hiyo, baadhi ya mafanikio hayo ni kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki katika vituo vyake kutoka 230,000 hadi kufikia vifaranga 1,059,440 mwaka 2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 78.3.

Anaongeza kuwa Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kuwekeza katika ukuzaji viumbe maji hususan ufugaji wa samaki kwa kutoa elimu. Hadi sasa kuna wakuzaji viumbe maji 26,474 waliozalisha samaki tani 17,233 mwaka 2020 ikilinganishwa na wakuzaji viumbe maji 16,284 waliozalisha tani 10,000 mwaka 2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 72.3.

Anaendelea kusema kuwa Wizara imeendelea kuhamasisha na kuwezesha wananchi kuwekeza katika zao la mwani kwa kutoa elimu ya kilimo na kuongeza thamani kwa zao hilo ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 552.8 mwaka 2010 hadi tani 1,484 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 186. Pia, jumla ya wananchi 292 wamepatiwa elimu ya utengenezaji wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na zao hilo kama vile sabuni na shampoo.

Dkt. Madalla anasema kuanzishwa kwa Dawati la Sekta binafsi kumesaidia kuwaunganisha wafugaji wa samaki na taasisi za kifedha ambapo hadi sasa Wizara imewezesha vikundi 60 vya wakuzaji viumbe maji kwa kuwapatia mafunzo ya ufugaji bora wa samaki na utunzaji wa fedha.

Akizungumzia changamoto, Dkt. Madalla anasema kuwa changamoto iliyopo ni uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli za ukuzaji viumbe maji hasa uzalishaji wa vifaranga vya samaki ■



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Luhaga Joelson Mpina (wa kwanza kushoto) akiwa na baadhi ya watumishi na wadau wa Sekta ya Uvuvi, akikagua Kituo cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji cha Mwamapuli kilichopo Igunga mkoani Tabora.**

# DKT. TAMATAMAH AFURAHISHWA NA SEKTA BINAFSI

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah amefurahishwa na jitihada zinazoendelea kufanywa na sekta binafsi katika kuendeleza tasnia ya ukuzaji viumbe maji.

Dkt. Tamatamah alisema hayo mara baada ya kumtembelea mmoja wa wafugaji wa samaki kwa kutumia vizimba Bi. Loycana Mwidunda ambaye pia ni mmoja wa wamiliki wa shamba maarufu la 'Konga Farm' lililopo Wilaya ya Magu mkoani Mwanza.

Dkt. Tamatamah alifurahishwa na uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye shamba hilo ambapo alimpongeza Bi Mwidunda kwa kuunga mkono kwa vitendo jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ambaye mara nyingi husisitiza juu ya uchumi wa viwanda unaotegemea malighafi za ndani.

"Kwa kweli nimefurahishwa na uwekezaji huu na nitumie fursa hii kutoa wito kwa wawekezaji wengine kwenye sekta ya uvuvi, kuigeukia tasnia hii ya ukuzaji viumbe maji kwa sababu inalipa sana na faida yake inapatikana kwa haraka zaidi ukilinganisha na uvuvi wa asili" Alisema Dkt. Tamatamah.

Dkt. Tamatamah alisema kuwa hivi sasa Tanzania inazalisha tani 497,567 kwa mwaka kupitia uvuvi wa asili ambapo alitoa angalizo la kupungua kwa samaki kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yanaoendelea hivi sasa duniani.



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (wa kwanza kushoto) akitoa maelekezo kwa mfugaji wa samaki kwa kutumia vizimba Bi. Loycana Mwidunda baada ya kumtembelea kwenye shamba lake "Konga Farm" lililopo Wilaya ya Magu mkoani Mwanza hivi karibuni.**

"Lakini kwa hivi sasa msisitizo wetu mkubwa ni ufugaji wa vizimba kwa sababu una faida kubwa na kwa kutumia eneo dogo tu mfugaji anaweza kuvuna hata mara tatu zaidi ya huyu anayefuga kwa kutumia mabwawa" Aliongeza Dkt. Tamatamah.

Kwa upande wake Bi. Mwidunda alisema kuwa shamba lake kwa sasa lina uwezo wa kuzalisha samaki tani 24 kwa mwezi ambazo ni sawa na tani 300 kwa mwaka huku akiongeza kuwa wana mpango wa kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya soko ambayo ni makubwa.

"Moja ya jitihada tunazofanya ili kuhakikisha tunazalisha samaki wengi zaidi ni kutengeneza kitotoleshi cha kisasa kwa ajili ya kuzalishia vifaranga vitakavyotumika shambani mwetu na ziada kuuzwa kwa wafugaji wengine." Aliongezea Bi. Mwidunda.

Naye Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Nazael Madalla alisema kuwa idara yake ipo tayari kutoa msaada wowote wa kitaalam kwa mmiliki wa shamba hilo na kuwahimiza wafugaji wengine wa samaki kuiga mfano huo.

Dkt. Madalla aliongeza kuwa moja ya changamoto kubwa zilizokuwa zikiikabili tasnia ya ukuzaji viumbe maji ni upungufu wa vifaranga na chakula cha samaki. Hata hivyo, Serikali ilihamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika uzalishaji Vifaranga na Chakula. Kwa sasa nchi inajitosheleza katika uzalishaji Vifaranga na uwekezaji katika Viwanda vya Chakula unaoendelea ikiwa ni pamoja na Kiwanda kipya kilichopo Ukerewe ili kukidhi mahitaji.

"Lakini pia Wizara inaendelea kufanya upanuzi wa vituo vyake vya ukuzaji viumbe maji ambapo kwenye hili tayari ujenzi wa Kituo kikubwa cha Ukuzaji viumbe maji umeshaanza huko Chato na kituo hicho kinatarajiwa kuwa kitovu cha stadi zote za ufugaji wa samaki kwenye vizimba hapa nchini " Alimalizia Dkt, Madalla.

Hadi kutokea mwaka 2015 Tanzania ilikuwa inazalisha wastani wa tani 3,000 za samaki kwa mwaka. Kutokana na ongezeko la hamasa ya ufugaji wa samaki kwa kutumia mabwawa na vizimba, idadi hiyo iliongezeka hadi kufikia tani 18,000 kutoka mwaka 2019 ■



**Mkurugenzi idara ya ukuzaji viumbe maji WMUV, Dkt. Nazael Madalla (kushoto) akimueleza jambo katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah wakati wa ziara ya kumtembelea mfugaji wa samaki kwa kutumia vizimba Bi. Loycana Mwidunda Wilayani Magu Mkoa wa Mwanza hivi karibuni.**

# MWANI, DAGAA KUWEKEWA VIWANGO VYA UBORA

Kwa Miaka mingi mazao ya Mwani na Dagaa kama yalivyo mazao mengine yanayopatikana baharini yamekuwa tegemeo kubwa katika kujenga uchumi wa jamii ya watu wa ukanda wa bahari ya hindi na hata taifa kwa ujumla.

Takwimu zinaonesha kuwa asilimia zaidi ya 90 ya Wanawake wanaoishi katika maeneo ya Pwani wanajishughulisha na kilimo cha Mwani ili kujipatia kipato huku ikielezwa kuwa Zanzibar mpaka sasa inazalisha takriban tani 35,000 na ndio bidhaa ya pili inayosafirishwa kwa wingi kwenda nje ya nchi.

Pamoja na jitihada hizo za uzalishaji wa Mwani na Dagaa bado mazao hayo hayajafikia hatua kubwa ya kuiingizia Serikali mapato makubwa yanayostahili kwa sababu katika kipindi chote hicho cha uzalishaji wa mazao hayo, bidhaa zake zimekosa kutambulika ipasavyo katika soko la ndani hata la nje kwa kukosa alama ya viwango vya ubora na usalama.

Kufuatia changamoto hiyo ya muda mrefu, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango nchini (TBS) na Wadau wengine imeamua kuandaa alama ya viwango vya Kitaifa vya ubora na usalama kwa mazao hayo ya mwani na dagaa ili kuyaongezea thamani na kuweza kupata masoko ya uhakika nchini na hata nje ya nchi.

Wakati akifungua Mkutano wa Wadau kuhusu mjadala wa viwango vya mazao ya Dagaa na Mwani uliofanyika jijini Dar es Salaam Agosti 24, 2020, Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah alisema kuwa kutengenezwa na kuanzishwa kwa viwango vya kitaifa vya ubora na usalama wa mazao hayo ya uvuvi kutaimarisha na kukuza soko la kitaifa na kimataifa la bidhaa zinazotokana na mazao hayo ya uvuvi.

"Mazao ya Dagaa na Mwani kwa muda mrefu yamekuwa hayana viwango vya ubora jambo ambalo limekuwa likifanya bidhaa hizo kutokutambulika katika soko la kimataifa ndio maana sasa serikali imeamua kutengeneza viwango vya ubora vya mazao ya uvuvi hasa Daagaa na Mwani ili yaweze kupata masoko yenye uhakika ndani na nje ya nchi,"alisema Dkt. Tamatamah.

Alisema kuwa uvuvi wa dagaa pamoja na ukulima wa mwani ni muhimu kwa uchumi wa jamii inayoishi Pwani




**Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi (WMUV), Ezra Mutagwaba (kushoto) akiongea katika Mkutano wa Wadau kuhusu Mjadala wa Viwango vya Mazao ya Dagaa na Mwani uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Katikati ni Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah na Kulia ni Mwakilishi wa Mratibu wa Mradi wa SWIOFish, Daniel Nkondola.**

na taifa kwa ujumla huku akisema kuwa kilimo cha mwani peke yake kinawahusisha takribani wakulima elfu tatu (3000) wengi wao wakiwa ni wanawake.

“Kwa mwaka 2019/2020 kiasi cha tani 1449 za Mwani zilizalishwa na kati ya hizo, asilimia 10 zilitumika hapa nchini katika kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwemo sabuni na aslimia 90 zilisafirishwa kwenda nje ya nchi zikiwemo nchi za China, Marekani, Canada, Uingereza, Denmark na Ufaransa,”alifafanua Dkt. Tamatamah

Dkt. Tamatamah aliendelea kueleza kuwa kutokana na umuhimu huo ni dhahiri kwamba kuna haja ya kuwepo kwa viwango vya ubora na usalama ili wafanyabiashara waweze kuyafikia masoko mbalimbali duniani.

“ Kupitia mradi wa SWIOFish ulio chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) tumeweza kuandaa viwango viwili ambavyo ni TBS/AFDC 23 kwa ajili ya unga wa Dagaa na TBS/ AFDC (5714) kwa ajili ya Mwani mkavu,”alibainisha Dkt. Tamatamah

Afisa Viwango wa Shirika la Viwango la Tanzania (TBS), Roda Mwailiza alisema kuwa viwango hivyo viwili vitasaidia sana kukuza biashara ya mazao hayo kwa sababu mazao hayo yatakuwa na viwango vya ubora vitakavyotambulika kitaifa na kimataifa.

Aidha, alisema kuwa baada ya kukamilika kwa viwango hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kutoa elimu kwa wadau wa sekta ya uvuvi ili kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kutumia viwango hivyo vya ubora katika biashara zao.

Naye Mkulima wa Mwani, Wilayani Bagamoyo, Mzee Machao Ally Jingalao alisema kuwa hatua hiyo ya Serikali ya kutengeneza viwango vya ubora kwa ajili ya mazao hayo ya uvuvi ni hatua nzuri ya kuelekea uchumi wa viwanda.

“Naiomba serikali iongeze nguvu katika kuimarisha biashara hii ya mazao ya uvuvi kwani ikisimamiwa vizuri itasaidia sana kuiongezea mapato nchi na kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja,”alisema Jingalao

Meneja wa Kampuni ya Uwekezaji katika zao la Mwani, Mariculture, Roger Valle Morre aliiomba Serikali kulinda wawekezaji katika zao la Mwani dhidi ya watu wanaojiingiza katika biashara hiyo bila kuwa na vibali ■




**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wadau wa Uvuvi muda mfupi baada ya kufungua Mkutano wa Wadau kuhusu mjadala wa viwango vya mazao ya Dagaa na Mwani uliofanyika jijini Dar es Salaam leo Agosti 24, 2020. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi(WMUV), Ezra Mutagwaba. Kushoto ni Mwakilishi wa Mratibu wa Mradi wa SWIOFish, Daniel Nkondola.**

# KITUO KIKUBWA CHA UKUZAJI VIUMBE MAJI KUJENGWA CHATO

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia sekta ya Uvuvi imeikabidhi kampuni ya ukandarasi ya Serikali ya Corporation Sole Works Superintendent eneo na mkataba wa Ujenzi wa Kituo kikubwa cha Ukuzaji wa Viumbe Maji ili kazi hiyo ianze mara moja.

Makabidhiano hayo yaliyofanyika tarehe 08/07/2020 katika kijiji cha Rubambangwe kilichopo Wilaya ya Chato mkoani Geita yalifanywa na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah ambaye mbali na kubainisha kuwa kituo hicho kitakuwa ni kikubwa kuliko vyote vya kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji hapa nchini.

Dkt. Tamatamah alisema kuwa mradi huo utajumuisha ujenzi wa mabwawa yatakayokuwa na uwezo wa kutoa zaidi ya tani 10 kwa mwaka, jengo la vitotoleshi vya samaki ambalo litakuwa na uwezo wa kutoa vifaranga zaidi ya milioni mbili kwa mwaka. Kiwanda kidogo cha kutengeneza chakula cha samaki na chumba cha ubaridi kwa ajili ya kuhifadhia samaki.

Aliongezea kuwa mradi huo utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 3.07 mpaka kukamilika kwake na tayari Wizara ilishalipa fidia ya shilingi milioni 42 kwa wakazi waliokuwa wakifanya shughuli zao za kiuchumi katika maeneo hayo yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 28.

“Lakini pia hapa litajengwa darasa, bweni na ukumbi wa chakula kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakuzaji viumbe maji wanaohitaji kujifunza au kuongeza ujuzi wa taaluma hiyo kwa kozi fupi za wiki mbili au tatu” Alisistiza Dkt. Tamatamah.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Ukuzaji Viumbe Maji ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa kituo hicho, Dkt. Nazael Madalla alisema kuwa kituo hicho kitakuwa ni kitovu cha Stadi za ufugaji Samaki kwenye vizimba. Kitakuwa ni ufumbuzi wa changamoto ya elimu duni katika ufugaji Samaki.

“Kituo hiki kitahudumia mikoa yote inayozunguka kanda ya ziwa na maeneo jirani na ukanda huo na tutawafundisha wafugaji wa samaki, maafisa ugani wa fani ya ufugaji wa samaki na pia kitatumika kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wanaosoma katika ngazi mbalimbali huko vyuoni” Aliongeza Madala.

Dkt. Madalla alibainisha kuwa kituo hicho kitawasaidia kupata mwongozo wa kujenga vituo vingine katika maeneo yanayozunguka Ziwa Tanganyika, Nyasa na maeneo ya Pwani lengo likiwa ni kuhakikisha viwanda vyote vya kuchakata samaki vilivyopo nchini havikosi malighafi.



**Mkuu wa Wilaya ya Chato Mhe. Charles Kabeho akizungumza na ujumbe kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi na taasisi ya ujenzi ya Corporation sol uliofika ofisini kwake hivi karibuni kabla ya kuelekea kijiji cha Rubambangwe ambako kitajengwa kituo kikubwa cha kukuzia viumbe Maji.**



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dokta Rashid Tamatamah akionesha mipaka ya eneo kinapotarajiwa kujengwa kituo cha kukuzia viumbe hai katika kijiji cha Rubambangwe wilayani Chato hivi karibuni muda mfupi kabla ya kukabidhi eneo hilo kwa mkandarasi (Corporation Sol) ili aweze kuanza ujenzi wa kituo hicho.**

Naye Afisa Mtendaji wa kijiji cha Rubambangwe Bi. Restituta Majura alisema kuwa mradi huo utawanufaisha sana wakazi wa kijiji hicho kwani mbali na kutoa ajira kwa wananchi watakaoshiriki kwenye hatua ya ujenzi, pia wanatarajia kunufaika na uwepo wa barabara itakayoelekea eneo la mradi kwani pia itawasaidia kufika kwenye zahanati ya kijiji inayoendelea kujengwa hivi sasa.

Kabla ya kuelekea kwenye eneo la ujenzi wa kituo hicho, Dokta Tamatamah akiwa na timu yake ya wataalam kutoka Wizarani walifika ofisini kwa Mkuu wa Wilaya ya Chato Mhe. Charles Kabeho ambaye aliishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kupeleka mradi huo kwenye Wilaya yake na kuahidi kufuatilia kwa ukaribu hatua zote za ujenzi wa kituo hicho hadi kitakapokamilika mnamo mwezi Oktoba mwaka huu ■



**Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dokta Rashid Tamatamah (kulia) akikabidhi mkataba na michoro ya majengo ya kituo cha kukuzia viumbe maji kwa Meneja wa Kampuni ya Corporation Sole Works Superintendent Bw. Simeo Machibya hivi karibuni Wilayani Chato (Geita).**

# UFUFUAJI WA TAFICO WAZIDI KUPIGA HATUA

Kufufuliwa kwa TAFICO kutawezesha Taifa kuzifikia, kuzimiliki na kunufaika na rasilimali za Uvuvi za Kitaifa hasa zilizopo Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ambazo Tanzania haijawahi kuzifikia tangu kupata uhuru

Moja ya mipango ya Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kufufua Shirika la Uvuvi- TAFICO (Tanzania Fisheries Corporation) ili kuiwezesha nchi kunufaika na rasilimali za uvuvi, hususan zile zilizopo katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu.

Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka ya 2020/2021 ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliyowasilishwa Bungeni na Waziri Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) katikati ya Mei, 2020 ilieleza kuwa imeshaandaa mpango biashara wa shirika hilo kwa lengo la kutoa mwelekeo wa kibiashara wa Shirika kwa kipindi cha miaka kumi (10).

Meneja Mkuu wa TAFICO, Ester Mulyila kupitia makala hii anafafanua hatua zilizofikiwa na Serikali mpaka sasa katika kuhakikisha Shirika hilo linatoa mchango unaotarajiwa.

Akitoa ufafanuzi huo kwa mtindo wa maswali na majibu alikuwa na haya ya kusema;

Tangu Mhe. Rais Dkt. John Magufuli atoe maelekezo ya kufufuliwa kwa Shirika la TAFICO mwaka jana mmefikia hatua gani mpaka sasa?

Mulyila anasema Ufufuaji wa TAFICO na kuwezesha uzalishaji wake ni muhimu kwa Sekta ya Uvuvi katika kufikia lengo linaloendana na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 2020 ya kununua meli za uvuvi zenye uwezo wa kuvua katika Ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu (Exclusive Economic Zone - EEZ) kwa lengo la kukuza uchumi na kuzalisha ajira nchini.

## Utekelezaji wa Maelekezo hayo

Anasema kufuatia Maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt.. John P. Magufuli ya kuharakisha kufufua TAFICO aliyoyatoa Disemba 12, 2019 wakati akihutubia Kikao cha Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mwanza, Wizara kupitia Menejimenti ya Kusimamia Taratibu za Kufufua TAFICO imeendelea kutekeleza malengo na mipango mbalimbali ikiwemo Kuwasilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri wa Kufufua TAFICO kutakakopelekea kufufua TAFICO kisheria, Kuhakiki mali za TAFICO, Kununua meli za Uvuvi katika Maji ya Ndani (Territorial waters) na Uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ), Kukarabati Miundombinu na Majengo ya TAFICO ikiwemo Majengo ya Ofisi, Mitambo ya Baridi ya Kuhifadhia Samaki (Cold Storage), Mitambo ya Kuzalisha Barafu, Karakana za Uhandisi mitambo na Zana za Uvuvi, pamoja na Ghati ya kuegeshea Meli za Uvuvi.

Anaendelea kufafanua kuwa kazi ya kuhakiki mali za TAFICO imekamilika kwa upande wa Dar es Salaam ambapo viwanja, majengo na miundombinu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 118.013 zimeainishwa na kuwa chini ya Serikali.

Jumla ya viwanja (Plots) saba (7) kati ya nane (8) vyenye nyumba za makazi tano (5); maghala mawili (2); na Ofisi



**Kaimu meneja wa shirika la Uvuvi nchini (TAFICO), Bi. Ester Mulyila akielezea maendeleo ya ufufuaji wa shirika hilo ofisini kwake Kigamboni, jijini Dar es salaam hivi karibuni.**

vimeainishwa na kuhakikiwa katika Mkoa wa Dar Es Salaam.

Menejimenti ya TAFICO imefanikiwa kufuatilia katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwezesha kupatikana kwa ufumbuzi wa utata uliojitokeza kwa nyumba ya Kurasini. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kanda ya Dar es Salaam imethibitisha Umiliki wa TAFICO kwa eneo na nyumba na hivyo kuwezesha kuokoa mali yenye thamani ya shilingi Bilioni 3.82.

Kwa maeneo nje ya Dar es salaam ikiwemo Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara, Mwanza na Kigoma utambuzi na uainishaji wa awali wa mali za TAFICO umekamilika.

Hata hivyo, kutokana na mali hizo kutumiwa na taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi, Wizara inaendelea na uhakiki kwa kushirikiana na taasisi zilizo nje ya Wizara ikiwemo Ofisi ya Msajili wa Hazina.

## Upatikanaji wa Fedha za Kufufua na kuwezesha TAFICO kuanza uzalishaji

Mulyila anasema Menejimenti kwa kushirikiana na Wizara imeendelea kutafuta vyanzo vya fedha ikiwemo kufanya mazungumzo na Wadau mbalimbali wa maendeleo ili kuona uwezekano wa upatikanaji wa fedha za kuiwezesha TAFICO kuanza uzalishaji. Wadau hawa ni pamoja na IFAD ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 68 zimeombwa kwa ajili ya kununua meli za Uvuvi katika Bahari Kuu pamoja na ukarabati wa miundombinu ya TAFICO, Benki ya Dunia wanaofadhili Mradi wa SWIOFish unaoendeshwa na Wizara kwa lengo la kupata fedha ya ukarabati wa miundombinu ya TAFICO pamoja na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).

“Menejimenti kwa kushirikiana na Wizara imefanikisha upatikanaji wa fedha ambapo Serikali ya Japan imetoa Msaada wa Yen Milioni 200 takriban Shilingi Bilioni 4.2 kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (Economic and Social Development Programme ESDP) kuiwezesha TAFICO kupata vifaa vya uvuvi. Vifaa vitakavyonunuliwa na Serikali ya Japan ni pamoja na meli moja ya uvuvi pamoja na nyavu zake, mtambo wa kuzalisha barafu (ice plant), Ghala la baridi la kuhifadhia samaki (cold storage), vifaa vya karakana ya uhandisi, pamoja na gari maalum lenye mitambo ya ubaridi (refrigerated vehicle). Kupitia programu hii Serikali ya Japan itanunua, itasafirisha, itasimika mitambo katika eneo la Ras Mkwavi na kufundisha juu ya matumizi ya mitambo hiyo, anasema

“Mnamo tarehe 27 Disemba 2019 Serikali ya Tanzania imetiliana sahihi na Serikali ya Japan kuanza utekelezaji wa program hiyo. Mpaka sasa taratibu za manunuzi ya vifaa pamoja na uundaji wa meli ya uvuvi zimeanza kupitia programu ya ESDP,anaongeza

Meneja huyo anasema Wizara kupitia Menejimenti ya Kusimamia Taratibu za Kufufua TAFICO imefanikisha maandalizi na kukamilisha Mpango wa Biashara (Business Plan) wa TAFICO kwa kipindi cha miaka kumi (10) kuanzia 2020. Mpango ambao umebainisha mahitaji ya jumla ya Shilingi 89,282,057,278.

Mpango huo umeainisha jumla ya miradi kumi (10) inayotegemewa kutekelezwa ambayo imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo:-

(a) Uvuvi (i) Uvuvi katika ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu kwa Meli ya mshipi (Long liner); (ii) Uvuvi katika ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu kwa Meli ya wavu (Purse Seiner); (iii) Meli ya Uvuvi katika Maji ya Kitaifa; (iv) Mtambo wa kuzalisha barafu; na (v) Ghala la baridi la kuhifadhia samaki (Cold Storage Facility);

(b) Uchakataji - kupitia Viwanda vya Uchakataji wa samaki na mazao yake; na

(c) Ukuzaji viumbe maji (i) Mtambo wa Kutotolesha vifaranga vya samaki (hatchery); (ii) Mashine ya Kuzalisha chakula cha samaki; (iii) Ufugaji wa samaki kwenye mabwawa; na (iv) Ufugaji wa samaki kwenye vizimba.

Mpango huo wa TAFICO unaotegemewa kutumiwa na Serikali na wadau mbalimbali ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Washirika wa Maendeleo kama vile IFAD na Benki ya Dunia utawezesha upatikanaji wa fedha za kuanzisha uzalishaji katika miradi pamoja na uendeshaji wa TAFICO.

Kuhusu Muundo wa TAFICO, Mulyila anasema mahitaji ya sasa ya Shirika na ya Kisekta umeandaliwa na tayari umewasilishwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao unaonesha mtiririko wa utekelezaji wa majukumu ya TAFICO katika maeneo ya kiufundi ya Uvuvi, Ukuzaji viumbe maji na Uchakataji wa samaki pamoja na Utawala na mahitaji ya rasilimali watu.

## Kudhibiti Kubomoka kwa Jengo la Ofisi kwa Mmonyoko

Akizungumzia jitihada zilizofanywa katika kutunza mazingira anasema, Wizara kupitia Menejimenti ya TAFICO imekamilisha Ujenzi wa kutunza ardhi (Earth Protection) ili kuzuia Jengo Kuu la Ofisi za Ras Mkwavi lisibomoke. Gabions zenye upana na urefu wa mita moja zimejengwa na kudhibiti mmomonyoko na mporomoko wa ardhi katika eneo la ardhi lenye kina cha mita 12 katika upana wa mita 20 ili kuokoa Jengo lisibomoke. Kazi hiyo ilikuwa ni pamoja na kujaza mawe na kifusi kuziba shimo katika uvungu wa jengo lililoachwa wazi na mmomonyoko na mporomoko wa ardhi. Anasema ujenzi huo umenusuru jengo la Ofisi ya Utawala la TAFICO kutokana na tishio la kubomoka.

## Uwepo wa TAFICO Utasaidia nini katika harakati za Serikali kuelekea uchumi wa viwanda?

Mulyila anasema Shirika la Uvuvi Tanzania TAFICO litakuwa na Meli za kitaifa (National Fleet) zitakazofanya uvuvi wa kibiashara wenye tija hususan Uvuvi wa Jodari (Tuna) katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) pamoja na Maji ya Kitaifa na kuiwezesha Serikali kuongeza mapato kutokana na Uvuvi huo.

“Uwepo wa TAFICO katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ), utawavutia wawekezaji binafsi hasa wa ndani ya nchi kuwekeza katika ukanda huo na nchi kunufaika na uvuvi wa Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ), anasema.

Anaendelea kueleza kuwa Shirika la Uvuvi Tanzania TAFICO litakuwa na viwanda vya uchakataji samaki na mazao yake ili kuongeza thamani katika mnyororo wa thamani kwa biashara ya samaki.

"TAFICO itakuwa na miradi ya Ukuzaji viumbe maji (aquaculture) hususan kuwa na Kitotoleshi (hatchery) cha kuzalisha vifaranga bora vya samaki wa kufugwa, kiwanda cha kuzalisha chakula bora cha samaki wafugwao pamoja na ufugaji wa samaki kwenye mabwawa na vizimba ili kuongeza uzalishaji wa samaki unaotokana na ukuzaji viumbe maji,anaeleza

Anasema kuwa Samaki watokanao na uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ), uvuvi katika Maji ya Kitaifa pamoja na watokanao na ufugaji samaki watachangia kuwa mali ghafi katika viwanda vya uchakataji samaki na mazao yake na kuiwezesha Serikali kuongeza mapato.

"Inatarajiwa kuwa TAFICO itakuwa na mchango mkubwa katika kufikia azma ya Serikali ya awamu ya tano ya kuelekea kwenye uchumi wa viwanda kwa kuongeza upatikanaji wa chakula na lishe, malighafi kwa ajili ya viwanda, kuongeza ajira kwa watanzania, kuinua kipato na kukuza uchumi wa Taifa kwa ujumla,anafafanua

"Taifa letu litaweza kuzifikia, kuzimiliki na kunufaika na rasilimali za Uvuvi za Kitaifa hasa zilizopo Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ambazo Tanzania haijawahi kuzifikia tangu kupata uhuru,anaeleza

## Ni Mafanikio gani ya kujivunia mliyoyafikia mpaka sasa?

Akieleza kuhusu mafanikio yaliyofikiwa na Shirika hilo mpaka sasa anasema Mali hususan viwanja (plots), majengo na miundombinu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 118.013 vimerejeshwa chini ya Serikali huku mali yenye thamani ya shilingi Bilioni 3.82 kufuatia ufumbuzi wa mgogoro (eneo na nyumba ya Kurasini) na uthibitisho wa Umiliki wa TAFICO toka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kanda ya Dar es Salaam zikiokolewa.

Mulyila anaeleza kuwa Menejimenti kwa kushirikiana na Wizara imeendelea na mazungumzo na IFAD ambapo mazungumzo hayo yamepelekea ngazi ya Usanifu (Designing) wa Programu ya Agriculture and Fisheries Development Programme (AFDP) ambapo meli mbili (2) za Uvuvi katika Bahari Kuu zinatazamiwa kununuliwa.

Wakati huohuo anaeleza kuwa tayari Serikali ya Japan imetoa Yen Milioni 200 takriban Shilingi Bilioni 4.2 kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (Economic and Social Development Programme ESDP) kununua meli ya uvuvi ya TAFICO pamoja na vifaa vingine vya uvuvi na taratibu za manunuzi na uundaji wa meli zimeanza.

"Mpango wa Biashara (Business Plan) wa TAFICO kwa kipindi cha miaka kumi (10) kuanzia 2020 umekamilika tayari kwa matumizi. Mpango wa Biashara huo uliobainisha mahitaji ya jumla ya Shilingi 89,282,057,278 ni hatua muhimu ya kuiwezesha TAFICO kuanza uzalishaji, alisema

## Ni Changamoto gani ambazo Shirika inakabiliana nazo?

Mulyila anasema kuwa changamoto kubwa ni uchakavu wa majengo ya Ofisi na miundombinu, uchakavu huo unatokana na majengo na miundombinu hiyo kukaa bila kutumika kwa takribani miaka 24 hivyo yanahitaji ukarabati mkubwa.

Changamoto nyingine anasema ni Mabadiliko ya Tabianchi yaliyosababisha eneo la Rasi-Mkwavi yalipo makao makuu ya TAFICO kuathiriwa sana na mmomonyoko wa ardhi hivyo jitihada zinahitajika kuyanusuru majengo pamoja na kiwanja ambacho vimeliwa kwa kiwango kikubwa na bado vinaendelea kuathiriwa na mmomonyoko wa ardhi.

Anaeleza kuwa kuathiriwa kwa Gati (floating jetty) na Tsunami Disemba 2005 kwa minyororo ya nanga kukatika imepelekea kutoka katika eneo lake hasa baada ya minyororo iliyobaki kukatika kwa kutu huku akiongeza kuwa uwepo wa Meli ya Ms Tawariq 1 iliyozama na kufungwa kwenye gati kunachangia uharibifu wa gati hivyo ukarabati wa ghati pamoja na kurekebisha mkao wake ni muhimu ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea endapo itazama.

Mulyila hakusita kuweka bayana changamoto ya upatikanaji wa fedha za kuendeshea Shirika hilo kutimiza azma ya kuanzishwa kwake huku akiendelea kufafanua kuwa Menejimenti inakabiliwa na uhaba mkubwa wa Rasilimali watu na ukosefu wa vifaa na vitendea kazi vya ofisi vya kuendesha shughuli za kila siku za Shirika.

## Wito wake kwa Wavuvi na Wadau wa Sekta ya Uvuvi kwa ujumla?

Mulyila anasema Shirika la TAFICO litaendesha miradi mbalimbali ambayo itaendeshwa kwa mfumo wa ubia na Sekta binafsi hivyo Wavuvi na jamii kwa ujumla watumie fursa hiyo kutimiza malengo yao.

"Baadhi ya miradi itakayoendeshwa na Shirika la TAFICO inalenga kutoa huduma kwa jamii kama vile upatikanaji wa barafu na huduma za uhifadhi samaki ili kuboresha ubora wa mazao ya uvuvi na kupata bei nzuri hivyo nawashauri Wadau wa uvuvi na jamii kwa ujumla watumie fursa hiyo,anasema

Anasema Wavuvi wanashauriwa kutotumia zana haribifu ili kuwa na uendelevu wa rasilimali ya uvuvi na Uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali kupitia TAFICO kuwa na manufaa endelevu.

Aidha, Wavuvi wanashauriwa kujiunga ili kupata nguvu ya kuwekeza zaidi katika uvuvi wa Bahari Kuu na katika kuongeza thamani katika mnyororo wa mazao ya uvuvi na kuitumia fursa ya uendeshaji wa Shirika kwa ubia.

"Jukumu la Kufufua TAFICO ni kubwa na linahitaji ushirikiano katika kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha na rasilimali watu ya kutosha ili ndoto iliyokusudiwa ya kuwa na Tanzania ya Viwanda hususani katika Sekta ya Uvuvi iweze kutimia kupitia shirika hili. Kwa kufanya hivyo Mchango wa sekta ya Uvuvi katika GDP utaongezeka, ajira zitaongezeka na kuweza kupunguza umaskini nchini,alibainisha ■



Jarida hili la Mtandaoni hutolewa na

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
**Wizara ya Mifugo na Uvuvi,**
S.L.P. 40487, Dodoma,Tanzania
Email: ps@mifugo.go.tz / ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: www.mifugouvuvi.go.tz